


UKURASA 3

## CCM yawaita wapinzani kuipa ushauri upungufu wa kiutendaji





# Nipashe

Jumatatu Februari 27, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581234

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


UKURASA 11

# PANGA LAPITA

**MABADILIKO** ya nne yagusa Baraza la Mawaziri, RC, makatibu wakuu...*Endelea ukurasa 2*




Hamisi Mwinyijuma
NAIBU WAZIRI MICHEZO


Cyprian Luhemeja
NAIBU KATIBU MKUU- MAJI


Abdallah Ulega
WAZIRI WA MIFUGO


Christina Mndeme
MKUU WA MKOA SHINYANGA


Dk Fracis Michael
MKUU WA MKOA SONGWE


Ramadhan Kailima
MKURUGENZI WA NEC


Omary Mgumba
AMETENGULIWA


Mashimba Ndaki
AMETENGULIWA

# ACT waibuka na madai mazito uwanja wa ndege

UKURASA 4

UKURASA WA 2

## AUAWA, MWILI WAKE WATUPWA BARABARANI

ZIADA Jafari (40), mkazi wa Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara amekutwa ameuawa na mwili wake kutupwa pembezoni mwa barabara.

Akithibitisha kutokea kwa mauaji hayo jana mkoani Mtwara, Kaimu kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Hamisi Ramadhamani, alisema tukio hilo lilitokea juzi wilayani hapa majira ya sita usiku...

UKURASA WA 3

## MWANAFUNZI, RAIA WA KENYA WADAIWA KUJINYONGA TARIME

WATU wawili wanadaiwa kujinyonga katika matukio tofauti mjini Sirari na Kijiji cha Kubiterere, akiwamo Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Nyansinsina, Kata ya Regicheri, Christina Edward. Mbali na mwanafunzi huyo, pia kuna kifo cha Tino Happy Onyango mwenye umri wa kati ya miaka 28 hadi 35 anayedaiwa kuwa raia wa Kenya, anayedaiwa kukutwa amejinyonga ndani ya chumba kwenye nyumba...

UKURASA WA 7

## WAFIKISHWA KORTINI KWA KUSHINDWA KUREJESHA MIKOPO YA HALMASHAURI

VIKUNDI 37 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi vimefikishwa mahakamani kwa kushindwa kurejesha Sh. milioni 61.5 ambazo ni fedha za mikopo itokanayo na asilimia 10 za mapato ya ndani ya halmashauri.

Kaimu Mkuu Idara ya Maendeleo...

## Siri kasi ya ongezeko la 'single mothers' yafichuliwa

UKURASA 5

MICHEZO ROBERTINHO AANIKA SIRI KUICHAPA VIPERS UK. 24 KATUNI UK. 6



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Solar Energy katika kituo cha mafuta cha Oryx Mwenge jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Anayeshuhudia ni Mkurugenzi wa Oryx Energy's Tanzania Limited, Kalpesh Mehta. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Panga la Samia lapita

**Na Mwandishi Wetu**

PANGA limepita! Katika kile kinachoweza kutafsiriwa kufanyiwa kazi kauli yake ya mwishoni mwa mwaka jana wakati wa Mkutano Mkuu wa CCM jijini Dodoma, Rais Samia Suluhu Hassan amefanya mabadiliko madogo kwenye Baraza lake la Mawaziri, makatibu wakuu na wakuu wa mikoa na taasisi za serikali.

Katika mabadiliko hayo, baadhi ya watendaji wamewekwa na wengine kupandishwa kwenye nafasi za juu zilizokuwa zinashikiliwa na mabosi wao.

Ni pangua pangua ya nne kwenye baraza tangu Rais Samia aingie madarakani Machi 19, 2021, mabadiliko hayo yakifanyika siku 12 tangu ulipotangazwa uteuzi mpya wa mawaziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Katika uteuzi uliofanyika jana, maofisa wanne wa Ofisi ya Rais, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Meneja wa NEMC Kanda ya Kati, wameteuliwa kuwa Manaibu Katibu Mkuu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma jana na Ikulu, Rais amehamishia majukumu ya uwekezaji katika Ofisi ya Rais huku akifuta nafasi ya Katibu Mkuu Uvuvi na badala yake Wizara ya Mifugo na Uvuvi itakuwa na Katibu Mkuu mmoja na wasaidizi wawili.

Taarifa hiyo iliyotiwa saini na Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Moses Kusiluka, ilibainisha kuwa aliyekuwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, anachukua nafasi ya aliyekuwa bosi wake, Mashimba Ndaki ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

Mbunge wa Jimbo la Muheza, Hamis Mwinjuma maarufu Mwana FA, ameteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, akichukua nafasi ya Pauline Gekul aliyehamishiwa Wizara ya Katiba na Sheria.

**WALIOHAMISHWA**

Rais Samia amewahamisha wizara; Pauline anayekwenda Wizara ya Katiba na Sheria, nafasi iliyokuwa inashikiliwa na Godfrey Pinda anayekuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Ridhiwani Kikwete amehamishwa kutoka Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwenda kuwa Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Deogratius Ndejembi amehamishwa kutoka Ofisi ya Rais Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwenda kuwa Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), nafasi iliyokuwa inashikiliwa na David Silinde aliyehamishiwa kuwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

**WAKUU WA MIKOA**

Rais Samia pia amemteuwa Christina Mndeme kuwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, akichukua nafasi ya Sophia Mjema aliyeteuliwa hivi karibuni kuwa Katibu wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi-Itikadi na Uenezi.

Vilevile, aliyekuwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Fransis Michael ameteuliwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe huku aliyekuwa Mkuu wa Mkoa huo akipelekwa mkoani Tanga kuchukua nafasi ya Omary Mgumba ambaye uteuzi wake umetenguliwa

**MAKATIBU WAKUU WAPYA**

Rais Samia ameteua makatibu wakuu wapya na wizara zao kwenye mabano; Dk. Tausi Kida (Ofisi ya Rais Uwekezaji), Juma Mkomi (Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) na Balozi Samweli Shelukindo (Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki).

Wengine ni Prof. Carolyne Nombo (Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia), Gerald Mweli (Wizara ya Kilimo), Dk. Seif Shekalaghe (Wizara ya Afya), Nadhifa Kemikimba (Wizara ya Maji), Kheri Mahimbali (Wizara ya Madini) na Mohamed Abdulla Khamis (Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari).

**WALIOBADILISHWA WIZARA**

Rais Samia pia amewabadilisha wizara makatibu wakuu watano ambao ni Prof. Riziki Shemdoe aliyetoka Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwenda Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. John Jingu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) kwenda Wizaya ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Wengine ni Dk. Jim Yonazi kutoka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwenda Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), huku Adolf Ndunguru akitoka Wizara ya Madini kwenda Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Anthony Sanga ametoka Wizara ya Maji kwenda Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**MANAIBU KATIBU WAKUU WAPYA**

Katika uteuzi huo Rais Samia pia ameteua manaibu makatibu wakuu wapya, akimteua aliyekuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Wilson Mahera kuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Afya).

Pia amemteua aliyekuwa Ofisa Mwandamizi Ofisi ya Rais Ikulu, Sospeter Mtwale kuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI, huku aliyekuwa Meneja wa NEMC Kanda ya Kati, Dk. Franklin Rwezimula akiteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekonolojia (Elimu ya Msingi na Sekondari).

Rais Samia pia amemteua Ofisa Mwandamizi Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Hussein Omari kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo huku aliyekuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Cyprian Luhemeja akiteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji.

Pia aliyekuwa Mkurugenzi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Lucy Kabyemera, ameteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wizarani humo, huku aliyekuwa Ofisa Mwandamizi Ofisi ya Rais Ikulu, Andrson Mutatebwa, akiteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maliasilia na Utalii.

Rais Samia amemteua aliyekuwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani, Athuman Mbuttuka, kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati huku akimteua Msajili wa Bodi ya Nyama Tanzania, Dk. Daniel Mushi, kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Pia amemteua aliyekuwa Mkurugenzi katika Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Agnes Meena, kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi huku aliyekuwa Ofisa Mwandamizi Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Selestine Kakele, akiteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

**MANAIBU WALIOHAMISHWA**

Katika uteuzi huo, Manaibu Makatibu Wakuu wawili wamehamishwa wizara ambao ni Dk. Grace Maghembe aliyekuwa TAMISEMI sasa anakwenda Wizara ya Afya na Nicholas Mkapa aliyekuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwenda Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**NEC**

Rais Samia pia amemteua Ramadhani Kailima kuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi akichukua nafasi ya Mahera aliyeteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu - TAMISEMI.

"Viongozi wote walioteuliwa katika nafasi mpya pamoja na naibu mawaziri waliohamishwa wizara, wataapishwa kesho (leo) saa 10 jioni, Ikulu Chamwino, Dodoma," ilibainisha taarifa hiyo ya Ikulu.

## Auawa, mwili wake watupwa barabarani

**Na Hamis Nasiri,**
MASASI

ZIADA Jafari (40), mkazi wa Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara amekutwa ameuawa na mwili wake kutupwa pembezoni mwa barabara.

Akithibitisha kutokea kwa mauaji hayo jana mkoani Mtwara, Kaimu kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Hamisi Ramadhamani, alisema tukio hilo lilitokea juzi wilayani hapa majira ya sita usiku.

Alisema kuwa Ziada alikuwa mkazi wa wilaya ya Masasi na ameuawa na watu ambao hawajafahamika huku mwili wa mwanamke huyo ukitupwa pembezoni mwa barabara.

Kaimu Kamanda huyo alisema uchunguzi wa awali kuhusu kifo cha mwanamke huyo umebaini kimetokana na kukosa hewa.

Alisema inaonyesha alikabwa hadi kukosa hewa na kupelekea umauti wake.

Alisema mwili wa marehemu umeokotwa kwenye barabara kuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kuelekea ofisi za Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) Kanda ya Kusini.

Kaimu Kamanda huyo alisema Jeshi la Polisi mkoani Mtwara linaendelea na uchunguzi wa tukio hilo na kwamba wahusika lazima wakamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Katika hatua nyingine, Kaimu Kamanda huyo alisema watu 18 wanashikiliwa na jeshi hilo kwa tuhuma mbalimbali za uhalifu ikiwamo uzembe na uvivu.

Alisema watuhumiwa hao wanatarajia kufikishwa mahakamani muda wowote kuanzia juma hili.

# CCM yawaita wapinzani kuipa ushauri upungufu kiutendaji

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar kimesema mlango upo wazi wa kupokea ushauri kutoka kwa wapinzani kama wataona kuna upungufu katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) inayoongozwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Naibu Katibu wa Idara ya Itikadi, Uenezi na Habari wa chama hicho, Khamis Mbeto Khamis, alitoa kauli hiyo alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika kwa mkutano wa Chama cha ACT-Wazalendo wa uzinduzi wa ahadi za chama hicho (Brand Promise) uliofanyika Hoteli ya Verde Zanzibar juzi.

"Serikali ya Umoja wa Kitaifa kama wakiona kuna upungufu, waeleze, sio kukaa pembeni kulalamika, CCM mlango upo wazi wa kupokea ushauri wao," alisema. Kiongozi huyo alisema serikali hiyo inaundwa na CCM na ACT-Wazalendo, hivyo Zanzibar itapata maendeleo makubwa kama suala la kuendelea kudumisha amani na umoja wa kitaifa litaendelea kupewa uzito.

Alisema mawaziri katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa wanafanya kazi vizuri, wakiwamo waliotoka ACT, akiwataka Nassor Ahmed Mazrui, Omar Said Shabani na Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman.

Mbeto alisema pamoja na serikali kuwa ya umoja wa kitaifa, wanatekeleza ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-25 ambayo imebeba mipango mbalimbali ya maendeleo inayoendelea kufanyika Zanzibar katika kipindi cha miaka mitano ijayo. "Wenzetu wanataka kuja kukamata serikali lakini sisi tayari tunaongoza na maendeleo makubwa yanaonekana katika sekta za elimu, maji, miundombinu na miradi mikubwa inayoendelea kutekelezwa katika visiwa vya Unguja na Pemba.

"CCM lengo lake kubwa ni kuona Mzanzibari anaishi maisha bora na lazima tudumishe amani na umoja wa kitaifa katika kufikia malengo hayo," alihimiza. Mbeto ambaye ameibua mjadala mkubwa Zanzibar baada ya kuhudhuria mkutano wa ACT-Wazalendo, akimwakilisha Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, alisema vyama vya siasa vitapita lakini nchi itabaki, hivyo kuwataka Watanzania kulinda misingi ya amani na mshikamano.

Kuhusu mambo mbalimbali yaliyoelezwa katika mpango wa ahadi ya ACT wa kuelekea uchaguzi mkuu, kiongozi huyo alisema kwamba mengi yamezungumzwa katika mpango wa CCM na yameshatekeleza na mengine yanaendelea kuyafanyiwa kazi.

"Waliyoyasema wao ACT, CCM inaendelea kutekeleza kupitia ilani yake ya mwaka 2020 na kila mwenye macho anashuhudia maendeleo hayo," alisema.

Aliongeza kuwa serikali ya awamu ya nane imejenga hospitali za kisasa katika kila wilaya na mkoa, shule za ghorofa 20 na shule za zamani zinaendelea kufanyiwa ukarabati pamoja na miradi mikubwa mitatu ya masoko ya kisasa inayoendelea kujengwa Mwanakwerekwe, Jumbi na Mbuzini.

Alisema serikali inaendelea kuimarisha huduma za maji, ikipa Sh. bilioni 34 Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ili kutekeleza mradi mkubwa maji.

Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT -Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema kwamba mpango wa ahadi wa chama hicho umelenga kuwapatia wananchi wa Zanzibar maisha bora iwapo chama hicho kitapewa dhamana ya kuongoza nchi.

Alisema lengo lao ni kuona Zanzibar inakuwa na mamlaka kamili ya kujiamulia mambo yake katika sekta tofauti badala ya mambo mengi kuwamo katika orodha ya mambo ya Muungano. "Tunataka Zanzibar mpya yenye katiba mpya, yenye uwajibikaji kwa sababu ndio ufanisi wa kuharakisha maendeleo kwa wananchi," alisema Zitto.

Akizungumzia mpango huo, Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud, alisema mpango huo umelenga kuonyesha njia ya kupita katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

"Lazima twende pamoja katika safari hii, Wazanzibari tungane bila ya kujali vyama, tuangalie Wazanzibari wanataka kwenda wapi na kama wapo katika chombo, lazima tujiulize tunakwenda wapi ili tufikie safari yetu ya kuleta maendeleo mapya ya Zanzibar.

"Chama cha ACT-Wazalendo ndio chombo cha kuwavusha wananchi katika kuwaondolea matatizo ya umaskini na kuwapatia maisha bora hasa katika upatikanaji wa huduma muhimu za jamii," alisema.



Mkurugenzi wa Masoko na Ukuzaji Biashara wa Benki ya TCB, Deogratius Kwiyukwa, akizungumza kwenye kikao cha watendaji mbalimbali pamoja mameneja wa matawi ya benki hiyo kwa ajili ya kujadili na kupanga mikakati ili kuboresha utendaji kazi jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Chongolo kutikisa Singida siku sita

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, anatarajia kuanza ziara ya siku sita leo mkoani Singida kwa ajili ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa kwenye halmashauri sita za mkoa huu kuona kama ilani inatekelezwa vyema.

Katibu Mwenezi wa CCM Mkoa wa Singida, Ahmed Kaburu, akizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapa, alisema kuwa katika ziara hiyo, Chongolo atafuatana na viongozi wa sekretarieti ya chama hicho taifa na ataanzia ziara wilayani Manyoni.

Alisema kuwa akiwa Manyoni, mtendaji huyo wa chama atatembelea na kukagua mradi wa maji Kintiku Lusilile, ujenzi wa sekondari ya wasichana Solya, ujenzi wa barabara ya Itigi-Rungwa, sekondari ya Itigi na kutembelea miradi ya chama na kuzungumza na wananchi.

Februari 28, mwaka huu, Chongolo atakuwa wilayani Ikungi ambako atatembelea Chuo cha Ufundi Stadi (VETA), ujenzi wa migodi wa Shanta Mining Limited, Hospitali ya Wilaya ya Ikungi, kufungua jengo la ofisi ya CCM wilaya na kuzungumza na wananchi.

Katika Wilaya ya Iramba ambako atakuwako Machi Mosi, Chongolo atatembelea zahanati ya Kinambue, Hospitali ya Wilaya, sekondari ya Lulumba, mradi wa maji Kiomboi na kuzungumza na wananchi.

Chongolo atatembelea Wilaya ya Mkalama Machi 2, akitarajiwa kutembelea sekondari ya Iguguno, Kituo cha Afya Kinyangiri, Hospitali ya Wilaya ya Mkalamba na kukagua ujenzi wa kituo cha polisi na kuhudhuria mkutano wa shina Iguguno.

# Mwanafunzi, raia wa Kenya wadaiwa kujinyonga Tarime

**Na Samson Chacha,** TARIME

WATU wawili wanadaiwa kujinyonga katika matukio tofauti mjini Sirari na Kijiji cha Kubiterere, akiwamo Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Nyansinsina, Kata ya Regicheri, Christina Edward.

Mbali na mwanafunzi huyo, pia kuna kifo cha Tino Happy Onyango mwenye umri wa kati ya miaka 28 hadi 35 anayedaiwa kuwa raia wa Kenya, anayedaiwa kukutwa amejinyonga ndani ya chumba kwenye nyumba ya kulala wageni mjini hapa.

Wakizungumza na Nipashe, wafanyakazi wa nyumba hiyo ya kulala wageni, Neema Joseph na Veronica Joseph walidai kuwa mgeni huyo alifika siku moja kabla kutokea kwa tukio hilo na kupewa chumba namba 14, lakini siku ya pili walipomgongea ili wafanye usafi, hakufungua mlango.

Alisema walichungulia dirishani na na kumwona mwanamke huyo akining'inia ndipo waliwajulisha polisi ambao walifika na kuvunja mlango.

Walidai kuwa baada ya kufungua, walibaini mwanamke huyo alijinyonga kwa kutumia kanga na hakuacha ujumbe wowote na kwamba polisi walichukua mwili kwa uchunguzi zaidi.

Katika tukio la pili, mwanafunzi wa kidato cha pili Shule ya Sekondari Nyansinsina anadaiwa kukutwa amejinyonga Februari 21 mwaka huu kwenye Kijiji cha Kubiterere

nyumbani kwa dada yake alikokuwa anaishi, sababu za kujinyonga hazijatajwa.

Diwani wa Sirari, Amos Sagara alisema tukio hilo limewashtua huku akiwataka wananchi wanapokumbwa na msongo wa mawazo, kuonana na wataalamu badala ya kujitoa uhai na kuacha majonzi kwa wanafamilia.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Tarime Rorya, Kamishna Msaidizi Geofrey Sarakikya alithibitisha kutokea kwa matukio hayo na kwamba wanaendelea na uchunguzi huku miili hiyo ikihifadhiwa kwenye chumba cha kuhifadhi maiti cha Kituo cha Afya Sirari.

Aliwataka wananchi kujitokeza kutambua mwili wa mwanamke huyo anayedhaniwa ni raia wa Kenya.

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
DODOMA DISTRICT REGISTRY
AT DODOMA
LAND NO. 32/2022
EDWARD ZEPHANIA NYEMBA & ANOTHER...............APPELLANT/APPL.
VERSUS
MAYAMAYA VILLAGE COUNCIL & OTHERS....................RESPONDENT
TO: CHICO INTERNATIONAL CO.LTD OF EVERYWARE

NOTICE OF DATE OF HEARING

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for hearing on **21 day of 3, 2023 at 9:00 am** Before **Hon G. J. MDEMU....JUDGE**
**YOUR ARE** required to appear in this court on the fixed date without fail. And you may bring with you all required documents in support of your case.
Given under my hand and the seal of the Court this **21 day of 2,2023**

DEPUTY REGISTRAR




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi (wa tatu kushoto), akimsikiliza Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim Tanzania, Jaffari Matundu (wa tatu kulia), akielezea huduma za benki hiyo kwa wadau wa utalii visiwani humo wakati Rais Mwinyi alipotembelea banda la benki hiyo katika mkutano wa wadau wa utalii Zanzibar (Z – Summit) mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT yaibuka na madai mazito uwanja wa ndege

**Na Waandishi Wetu,**
ZANZIBAR

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeanza rasmi mikutano yake ya hadhara Zanzibar kikimulika mambo matatu yanayolenga kutafuta kinachokiita maslahi mapana ya Zanzibar huku Kiongozi wake, Zitto Kabwe, akiendelea kupinga uamuzi wa serikali kuipa Kampuni ya DNATA uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, Terminal 3.

Akihutubia wanachama wa chama hicho katika mkutano uliofanyika jana Mkoa wa Kaskazini Unguja eneo la Nungwi, Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Zanzibar, Othman Masoud Othman, alionyesha kutoridhishwa na baadhi ya mambo yanayoendelea.

Akibainisha hoja hizo alidai kwa sasa Zanzibar imekuwa ni kama mlango wa duka linaloruhusu kila mmoja kutumia kupata faida na kisha kuondoka bila kujua maboresho yake yakoje.

Pia alidai kwa sasa Zanzibar wananchi wanaadhibiwa hata kwa kutumia mchanga ulioshushwa kwao na Mungu kwa kuwa maeneo mengi yamekodishwa kwa wawekezaji bila kujali wananchi wananufaika vipi.

"Dhana ya Zanzibar moja ni kutaka kuona viongozi wanawaunganisha wananchi na kuondoa dhana ya kuwa wachache ndiyo wenye haki kuliko wengine.

"Sisi tunaamini hii Zanzibar si ya ACT-Wazalendo, si ya CCM, si ya CHADEMA, ni ya Wazanzibari ambao wametoka maeneo mbalimbali bila kujali rangi, kabila wala dini, lakini hili leo limekuja kuvunjwa kwa sababu ya maslahi ya muda mfupi ya kisiasa," alisema Othman.

Katika hoja yake ya pili, aligusia madai ya kuchimba mafuta kwenye visiwa hivyo, akisema Zanzibar haiwezi kuchimba mafuta yaliyoko kwa kuwa hakuna sheria inayoruhusu jambo hilo kwa Wazanzibari.

Alisema ameamua kuongea ukweli huo hata kama baadhi ya watu hawapendi kusikia ukisemwa hadharani.

"Ili tuchimbe mafuta yetu Wazanzibar, ni lazima sheria ibadilishwe na kwa sasa hakuna sheria iliyobadilishwa ndiyo maana sisi ACT-Wazalendo, tunatakaa mamlaka kamili ya Zanzibar itakayokuja na sheria hiyo ya kuwanufaisha wananchi," alisema Othman.

Katika hoja yake ya tatu, kiongozi huyo alisema madai ya mamlaka kamili ya Zanzibar ni ya Wazanzibar wote, akidai kuwa wana CCM wanaona aibu kudai mamlaka hayo kwa hofu ya kupoteza nafasi zao za kisiasa.

Alisema hofu ya wana CCM kudai mamlaka kamili ya Zanzibar ni kutokana na hofu ya kunyimwa ujumbe wa kamati kuu, nafasi ya kuwania ujumbe au uwakilishi pamoja na nafasi nyingine za uteuzi.

Alibainisha kuwa dhana ya mamlaka kamili ni kuiwezesha Zanzibar iwe na uhuru wa kukopa kutoka katika mashirika ya kifedha, uhuru wake wa kikodi na kuwa na sarafu yake na kwamba ACT-Wazalendo itasimamia hilo.

Alieleza kuwa sababu ya kuweka bayana dhamira ya chama hicho ni kwa ajili ya kuondoa dhana ya kuwafikia wananchi wakati wa kampeni pekee, hali inayofanya washindwe kutafakari kwa umakini juu ya vyama vitarajie kuwafanyia nini vikipata madaraka ya dola.

**ZITTO KABWE**

Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Zitto, aliitaka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuiondoa Kampuni ya DNATA kutoka Dubai inayotoa huduma kwenye uwanja wa ndege, akidai kuna ukiukwaji wa sheria, hivyo watoe ushindani wa kibiashara.

Alidai sheria ya anga ya Muungano hairuhusu kampuni moja kuwa na ukiritimba kwenye eneo la biashara na jengo la abiria la terminal 3 kuendeshwa na kampuni moja ni kinyume cha sheria.

Zitto alidai sheria zinapaswa kuheshimiwa, hivyo chama cha ACT Wazalendo hakiwezi kunyamaza kimya wakati sheria zinavunjwa.

Alisema kwa mujibu wa sheria, kampuni za kigeni haziruhusiwi kuwa na hisa zinazozidi asilimia 65, hivyo lazima mamlaka, ikiwamo ya kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi Zanzibar, zinapasswa kuchunguza suala hilo.

Alisema hawawezi kukubali kuona ufisadi unafanyika katika nchi na hivyo wataendelea kuhoji wanapoona kuna viashiria vyake.

**MSHIKAMANO**

Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Addo Shaibu, alitoa wito kwa wafuasi wa chama hicho kusimama imara na kuendeleza mapambano na mshikamano ili wakamilishe matarajio yao ya kushika hatamu.

"Zanzibar ni mshirika mwenye haki sawa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo inastahili fursa sawa na Tanganyika (Tanzania Bara) katika kufaidi matunda ya Muungano," alisema Shaibu.

Naibu Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo Zanzibar, Nassor Mazrui, alisema wana nia thabiti na kila sababu ya kutafuta mamlaka kamili na kwamba wanataka viongozi watakaoiongoza Zanzibar kwa uadilifu wa hali ya juu.

"Hatutaki tena kuona vikosi vyetu vya ulinzi vinatuua na kutubakisha yatima katika nchi hii, hatutaki tena kuona wanapita katika majumba ya watu kupora na kuchukua mali za watu na kuwanajisi dada zetu na kuona Wazanzibar wanawekwa ndani bila sababu yoyote," alisema Mazrui.

# Wanawake wajipanga mchakato Katiba mpya

**Na Christina Mwakangale**

WANAWAKE wanaharakati kwa pamoja wameazimia kuja na ajenda za pamoja kujiandaa kwa mchakato wa upatikanaji wa Katiba Mpya ili kufanikisha malengo ya upatikanaji haki kwa kundi hilo.

Wanajopo wakizungumza kwa nyakati tofauti kwenye kongamano la kuadhimisha miaka 15 ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Udhamini wa Wanawake Tanzania (WFT-T), walisema mkoani Dar es Salaam mwishoni mwa wiki kuwa vuguvugu la utetezi wa wanawake linahitaji ushirikiano.

Mmoja wa wanajopo katika kujadili harakati wanawake nchini, mafanikio, matarajio na changamoto, Dk. Ave-Maria alisema baada ya ripoti ya kikosi kazi cha Rais kukusanya maoni, kumaliza kazi yake Oktoba mwaka jana, kati ya ajenda zilizopendekezwa ni mchakato wa Katiba Mpya.

"Ushauri huo uliotokana na maoni yaliyotolewa kwa kiwango kikubwa ni kikosi kuhusu mchakato wa Katiba Mpya. Tunafahamu mchakato uliishia njiani. Je, tunapoutarajia mpya, tumejipangaje kuja na ajenda za pamoja kama wanawake?

"Tumesikia mchakato maoni ya kikosi kazi, Katiba kama ipo njiani kutokana na maoni hayo, tunabeba vipi ajenda? Wakati wa Bunge la Katiba Mtandao wa Wanawake na Katiba-Ulingo, tulikuja na ajenda 12 na miongoni mwake 11 zilifanyiwa kazi.

"Kati yake, zimo kwenye Katiba pendekezwa ni haki sawa katika nafasi za uongozi, ulinzi wa utu wa mwanamke, utekelezaji mikataba ya kimataifa, haki za wasichana, wenye ulemavu, uzazi salama na umiliki wa rasilimali," alisema Dk. Ave-Maria, ambaye ni Mratibu wa Taifa wa Taasisi ya Ulingo. Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Msichana Initiative, Rebecca Gyumi, alisema mabadiliko kwenye jamii na ujenzi wa harakati, matokeo yake huchukua muda mrefu, hivyo ruzuku kwenye eneo hilo iwe endelevu.

"Wakati tuliona umuhimu wa ruzuku ili kuimarisha ajenda zetu, kuelimisha na kuondoa ukandamizaji wa haki, bado kunahitajika mabadiliko kwenye mifumo. Mfano, kwenye sheria, zipo sheria ambazo bado zinamnyima haki mtoto, msichana, hii ni pamoja na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 na maeneo mengine ya Katiba, inasababisha mfumo kandamizi," alisema Rebecca.

Oktoba mwaka jana, Mwenyekiti wa kilichokuwa kikosi kazi, Prof. Rwekaza Mukandala, alikabidhi ripoti hiyo kwa Rais Samia Suluhu Hassan ili mapendekezo kufanyiwa kazi katika masuala mbalimbali ya demokrasia na siasa.

Kati ya mapendekezo 18 yaliyotolewa, 16 yalihusu masuala ya kikatiba na mengine yakigusia ya usawa wa kijinsia na demokrasia, wakishauri umuhimu kuunda jopo la wataalamu ambao wataandaa rasimu ya Katiba Mpya kwa kuangazia mapendekezo ya sasa, pia kupitia rasimu ya pili ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba.




Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Bank of Africa, Nandi Mwiyombella (kushoto), akimwelezea Waziri wa Nishati, January Makamba, huduma zinazotolewa na benki hiyo, alipotembelea banda la maonyesho la benki kwenye mkutano wa Jukwaa la Biashara la Nchi za Ulaya na Tanzania uliofanyika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sababu wanaume kukwepa malezi ya watoto zatajwa

**Na Christina Mwakangale**

WANAHARAKATI ngazi ya jamii wamesema hali duni kiuchumi na mabadiliko ya mfumo wa maisha ni sehemu ya sababu za wanaume kutotoa huduma kwa familia zao hususan kwa watoto wanaohitaji chakula, malazi na mavazi.

Vilevile, imeelezwa kuwa mabadiliko ya mfumo wa maisha ambao hivi sasa wanawake walio wengi wanamudu gharama za kuishi kwa kufanya shughuli tofauti za kujipatia kipato, kumesababisha familia nyingi kuhudumiwa na wanawake.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam na wanaharakati, watetezi wa haki za binadamu na walezi wa jamii walipozungumza na Nipashe.

Mtaalamu wa Ustawi Jamii na Mshauri na Masuala ya Familia, Malezi na Makuzi ya Watoto na Malezi ya Vijana, Joseph Kayinga, alisema hivi sasa wanawake, hususan wanaoishi mijini, wanaonekana wanamudu kulea watoto wenyewe.

"Hii 'single mother' ni kama mtindo fulani ulioingia hivi sasa. Kinadada au kinamama wanahamasishana na kwamba hawataki usumbufu. Ukiulizia watoto walio wengi wenye uhalifu, wamekosa malezi ya pande zote mbili.

"Ila ukweli ni kwamba hata hao wanaume wasiolea wao wamelelewa vipi? Wengi ni ambao pia walikosa malezi ya wote. Siku hizi kuna nyimbo kama zimefadhiliwa, badala ya kuona ni tatizo, zinahamasisha kuachana kwamba hakuna gharama.

"Sasa hivi kuna wanawake wana fedha za kutosha, anamkodi tu mwanaume, ili apate naye mtoto. Binadamu ni mtu wa kuiga hao wanaolelewa na 'single mother' nao watapitia hayo hayo," alisema mtaalamu huyo wa ustawi wa jamii.

Hancy Obote, Mkuu wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Kata ya Sarnga, vinavyosimamiwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), alitaja sababu tatu tofauti zinazochangia wanaume kutolea watoto ambazo ni mfumo wa uchumi kubadilika, ukosefu wa ajira na hata kwenye sekta ya kujiajiri.

"Ajira hakuna, biashara ngumu na rundo la kodi na tozo mbalimbali, hili linafanya watu kukosa kipato na kuamua kuondoka kwenda kutafuta na mwisho anashindwa kurudi.

"Mitindo ya maisha na mwingiliano wa tamaduni, miaka ya 2000 kurudi nyuma wasomi walikuwa wachache na watu waliamini katika kazi za mikono na biashara, hivyo watu waliamini nguvu zao na waliweza kujitegemea mapema sana tofauti na sasa watu wengi ni wasomi wanaamini zaidi katika ajira," alifafanua.

Alisema wanaume walio wengi hukosa nguvu ya uchumi na kushindwa kujitegemea huku umri ukienda na kuamua kuoa kwa sababu tu umri umekwenda.

"Mwishowe ndoa ni majukumu, mtu anashindwa kuyamudu anakimbia. Kutokuelewa masuala ya haki na utetezi hasa masuala ya haki za wanawake, unakuta mwanaume anajituma kwa nguvu zote, mwanamke kwa sababu anajua jamii na sheria pamoja na harakati zipo upande wake, anaanza vurugu.

"Na sheria zinamwacha mwanaume kando, mwisho anajikuta yeye ni kama mtumwa tu katika familia, wengine wakisikia kesi za namna hii, wanaamua kuachia majukumu na wanawake kubeba mzigo, hii niliikuta Kigoma vijijini, wanaume wanashinda wanacheza bao.

"Nilipouliza, wanasema wao hawawezi kuwa watumwa wa wanawake, kwa sababu sheria zinawabeba sana wanawake na watoto, hawaoni mchango wa baba, hata akijituma utasikia 'nani kama mama?' na hata ikitokea kesi, watoto humtetea mama," alisema mwanaharakati huyo.

Mmoja wa mzazi wa kiume (jina tunalo), alisema alipata mtoto na mzazi mwenzake akiwa chuoni, hivyo alikuwa hajajipanga kwa ajili ya kulea mtoto kutokana na kutokuwa na kazi ya kumwingizia kipato.

"Mimi hadi leo nikwambie nina miaka 28, nimehitimu chuo kikuu na bado ninaishi na wazazi. Sio kwamba ninapenda, sipendi, ni kwa sababu sijapata kazi.

Sasa huyo mtoto fedha ya kumhudumia nitaitoa wapi wakati mimi mwenyewe ninahudumiwa?

"Unajua ni 'nature' (asili) tu mtoto ni wa mama, atakaa naye muda mwingi, hana jinsi. Ila ikishindikana kabisa ndipo utakuta baba anachukua mtoto na kumpa mama yake mzazi, yaani bibi alee, lakini si wanawake wote wapo radhi kumtoa mwanawe mdogo akalelewe na upande wa mwanamume," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, akizungumzia suala hilo, alisema kumejengekeza mfumo wa kutowajibika kwa baadhi ya wanaume licha ya kufahamu wana majukumu mbele yao.

Mkurugenzi huyo kupitia ripoti iliyotolewa na gazeti hili wiki iliyopita, alinukuliwa akisema: "Sheria ya jinai na madai inatoa wajibu wa baba kulea familia yake, kulea watoto wake, kizazi chake.

"Kuna sheria inalazimisha hivyo. Ingawa wanaotakiwa kufanya sheria itekelezeke wanakuwa 'walaini' kidogo, lakini inatakiwa kufuatiliwa kwa kina," alisema Anna.

Ripoti hiyo ya Nipashe ilibainisha kasi ya ongezeko la malezi ya upande mmoja, hasa kinamama kulea watoto peke yao 'single mothers' huku wanaharakati wakitaka sheria iliyoko iongezwe 'meno' ili kuwabana kinababa wasiowajibika kwenye malezi.

Nipashe imebaini kuna ongezeko kubwa la malezi ya upande mmoja ambayo yanatajwa kuchangia kuporomoka kwa maadili na ukatili dhidi ya watoto.

Gazeti hili pia limebaini watoto wenye umri kuanzia miaka mitatu na zaidi wanajilea kwenye baadhi ya barabara kuu, ikiwamo makutano ya Mwenge, Buguruni, Ubungo Darajani na eneo la Ubalozi, kwenye makutano ya barabara Ali Hassan Mwinyi na Kinondoni.

Watoto wa aina hiyo pia wamo kwenye masoko kadhaa ya Dar es Salaam, yakiwamo ya Mabibo, Kariakoo, Tegeta, Mbagala, Temeke na Buguruni.

# Majaliwa awabana ma-RC na ma-DC kilimo cha michikichi

**Na Mwandishi Maalum**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amewataka wakuu wa mikoa, wilaya na viongozi wa vyama vya siasa watumie majukwaa waliyonayo kuhimiza kilimo cha michikichi ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo nchini.

"Viongozi wote wa mikoa, wilaya na wa vyama vya siasa, mnayo majukwaa ya kukutana na wananchi kila wakati. Twendeni tukahamasishe wananchi walime michikichi kwa sababu ni zao litakalowapatia fedha kwa muda mrefu," alisema Waziri Mkuu jana alipozungumza na wadau wa zao la michikichi mkoani Kigoma kwenye ukumbi wa NSSF.

Wadau hao wanajumuisha wakulima, wazalishaji miche, wakamuaji mawese, viongozi wa vijiji, viongozi wa taasisi za fedha, viongozi wa wilaya, halmashauri na Mkoa wa Kigoma.

Majaliwa aliitisha kikao hicho ili kujadili changamoto zinalolikabili zao hilo na kujadiliana njia za kuliendeleza ili kuhakikisha nchi inakuwa na kiasi cha kutosha cha mafuta ya mawese, hatua ambayo alisema itasaidia nchi kuepuka kuagiza kiasi kikubwa cha mafuta kutoka nje ya nchi.

Aliwataka wakuu wa mikoa na wilaya wenye ardhi inayokubali zao hilo, wafanye hivyo mara moja kwa kuwa mbali na kuwapa fedha za uhakika, litaleta fursa ya ajira kupitia viwanda vinavyofunguliwa.

"Michikichi ni fursa, michikichi ni maendeleo, Ni fursa ya kuleta viwanda hapa Kigoma na kwenye mikoa mingine itakayolima zao hili. Michikichi ni uchumi, ni uchumi wa mtu mmoja mmoja na uchumi wa kitaifa," alisisitiza.

Akizungumzia kuhusu mahitaji ya mafuta ya kula nchini, Waziri Mkuu alisema: "Hivi sasa mahitaji ya mafuta nchini ni zaidi ya tani 650,000 huku uzalishaji ukikadiriwa kuwa tani 290,000 tu. Hivyo, kiasi cha tani 360,000, sawa na asilimia 55.4, huagizwa kutoka nje ya nchi na kuigharimu serikali takribani Sh. bilioni 470 kila mwaka. Tunahitaji hii fedha iendelee kutumika nchini," alisema.

Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Waziri Mkuu alisema serikali imedhamiria kumaliza tatizo la upatikanaji wa mafuta ya kula nchini kwa kufanya mageuzi makubwa katika mazao ya mafuta ikiwamo michikichi. "Mageuzi haya yanakwenda sambamba na kupanda miche mipya iliyoboreshwa ambayo ina uzalishaji mkubwa wa mafuta. Wana-Kigoma tuamue sasa hivi tupande michikichi kwa bidii," alisisitiza.

Serikali ilichukua hatua za makusudi za kuliingiza zao la michikichi kwenye orodha ya mazao ya kimkakati. Mazao mengine ya kimkakati ni pamba, tumbaku, kahawa, korosho, chai, mkonge, zabibu na alizeti.

Akimkaribisha Waziri Mkuu kuzungumza na wadau hao, Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde alisema wizara hiyo inaendelea na uzalishaji wa mbegu na miche bora ya michikichi aina ya TENERA inayotoa mafuta mara tatu zaidi ya aina ya DURA ambayo inalimwa na wakulima kwa takribani asilimia 90.

"Hadi kufikia Januari, 2023 TARI kwa kushirikiana na kampuni binafsi imezalisha jumla ya mbegu milioni 14.14. Kati ya hizi, mbegu milioni 11.59 zimezalishwa na TARI na mbegu milioni 2.54 zimezalishwa na kampuni binafsi zikiwemo FELISA, NDF na Yangu Macho Group Ltd," alisema.

Alisema kati ya mbegu milioni 14.14 zilizozalishwa, mbegu milioni 9.60 zimekwishasambazwa na kuoteshwa na taasisi mbalimbali zikiwamo JKT na Magereza, halmashauri zote nane za Mkoa wa Kigoma, halmashauri 25 za nje ya Mkoa wa Kigoma, vituo vya TARI na Wakala wa Mbegu za kilimo Tanzania (ASA).

Alisema kuwa hadi kufikia Januari, 2023 jumla ya miche 3,122,566 imepatikana ambapo miche 1,968,087 imegawiwa kwa wakulima ndani na nje ya Mkoa wa Kigoma.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga robo fainali CAF inawezekana lakini...

**WAKATI** wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, juzi walipata ushindi wao wa kwanza katika mechi tatu walizocheza hadi sasa, jana usiku watani zao wa jadi, Yanga wanaobeba dhamana ya kuipeperusha bendera ya nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika walishuka dimbani nchini Mali dhidi ya wenyeji wao, Real Bamako.

Huo ni mchezo wa tatu kwa Yanga na wa pili ugenini baada ya ule wa awali kupoteza kwa mabao 2-0 dhidi ya US Monastir ya Tunisia na kisha kurejea nyumbani na kushinda 3-1 dhidi ya TP Mazembe ya DR Congo katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kwa Simba, ambayo nayo ilianza kwa kichapo cha bao 1-0 ugenini nchini Guinea dhidi ya Horoya AC, yenyewe ilirejea nyumbani, Benjamin Mkapa na kuangukia kipigo kizito cha mabao 3-0 kutoka kwa Raja Casablanca ya Morocco kabla ya kwenda ugenini nchini Uganda na kushinda 1-0 dhidi ya Vipers.

Hata hivyo, bila kujali matokeo ya jana usiku kati ya Yanga na Real Bamako, bado tunaamini wawakilishi wetu hao wanachotakiwa ni kushinda tu michezo yao miwili ya nyumbani pasipo kuangalia wapinzani wao wanavuna nini katika mechi zao.

Kwa kundi la Simba, Raja Casablanca imefuzu hatua ya robo fainali kutokana na kufikisha alama tisa ambazo zinaweza kufikiwa ama kupitwa na timu mojawapo tu kati ya Simba, Horoya ama Vipers kutegemeana na matokeo yao, hivyo kwa kuzingatia kanuni ya kila kundi kupitisha timu mbili, Wamorocco hao tayari wanatiketi mkononi ya kusonga mbele.

Hivyo, hesabu zilizobaki kwa Simba kwanza ni kushinda mechi zake mbili za nyumbani dhidi ya Vipers na Horoya, lakini ikiombea Raja Casablanca iifunge ama kutoka sare dhidi ya miamba hiyo ya Guinea watakapokutana Jumanne ya wiki ijayo jambo ambalo linawezekana kutokea. Ikumbukwe Simba itamalizia mechi zake za hatua ya makundi ugenini dhidi ya Raja Casablanca, ambayo ilionyesha ubora wa hali ya juu zilipokutana Uwanja wa Benjamin Mkapa na wageni hao kuibuka na ushindi wa mabao 3-0, jambo ambalo haitakuwa rahisi kwa wawakilishi hao wa nchi kushinda, ingawa kwenye soka lolote linawezekana.

Kwa upande wa Yanga, bila kutazama matokeo yake ya jana usiku, bado nayo inachotakiwa kuhakikisha ni kushinda mechi zake mbili nyumbani dhidi ya Real Bamako na US Monastir kabla ya kwenda kumalizia ugenini nchini DR Congo dhidi ya TP Mazembe.


Kinachotakiwa kufanya kwa sasa ni wachezaji na benchi lao la ufundi kutazama kwa kina wapi wanapokosea kuweza kuibuka na ushindi ili kutorejea tena makosa katika mechi zijazo ambazo zinakwenda kuamua timu mbili kutoka katika kila kundi zitakazotinga robo fainali. Tunaamini kwa muda wa wiki nzima uliobaki kabla ya Simba, Yanga kucheza mechi zao zijazo za kimataifa, zinaweza kabisa kujipanga na kurekebisha makosa yaliyojitokeza michezo iliyopita, kisha kufanya vizuri zitakaposhuka Uwanja wa Mkapa Jumanne na Jumatano wiki ijayo.

Tangu michuano hiyo ya kimataifa imeanza msimu huu, tatizo kubwa kwa wawakilishi wetu hao limekuwa ni kushindwa kutumia nafasi wanazotengeneza kitu ambacho katika mashindano makubwa kama haya nafasi hizo hupatikana mara chache sana.

Kwa mantiki hiyo, mabenchi ya ufundi Simba, Yanga wanapaswa kutumia kipindi hiki kifupi kurekebisha kasoro hizo kwa kuwawezesha washambuliaji wao kuongeza umakini na zaidi kuwajenga kisaikolojia ili kuondoa papara wakati wanapokuwa ndani ya 18.

Tunataka kuona wawakilishi wetu wote wakifuzu hatua ya robo fainali na hili litawezekana tu kwa idara zote ndani ya klabu kuanzia kwa wachezaji, mabenchi ya ufundi hadi kwa mashabiki ambao ni wachezaji wa 12 uwanjani, kila mmoja akitimiza wajibu wake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwangwo

## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba mpeni muda Robertinho asajili wachezaji wake bora

**UKIMSIKILIZA** kwa makini Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, bila ya kuwa na presha ya timu kupata matokeo mazuri, kucheza soka la kuvutia, au kufuata mkumbo, utagundua kuwa ni mmoja kati ya makocha wenye vitu vingi vya kiufundi.

Ni kwa sababu tu amekuja kwenye timu ambayo kwa sasa wanachama na mashabiki wake wanaishi zile zama za Simba ya kina Emmanuel Okwi, Luis Miquissone, Rally Bwalya, Chris Mugalu, Gerson Fraga, Thadeo Lwanga, Meddie Kagere na wengine ambao waliifanya kuwa ya kutisha.

Wengi hawaamini kuwa Simba iliyokuwapo sasa siyo ile, bali inapitia kipindi cha kutengenezwa upya. Kwa bahati mbaya sana viongozi wa klabu hiyo walikuwa hawasomi alama za nyakati, badala yake madirisha mawili ya usajili walikuwa wanaleta wachezaji wa kwenda kuongeza nguvu ya wachezaji waliopo, badala ya kusajili watakaounda timu mpya kabisa.

Kwenye dirisha kubwa, mchezaji aliyeingia moja kwa moja kwenye kikosi ni Moses Phiri tu, na kwenye dirisha dogo ni Saido Ntibazonkiza pekee.

Lakini kwa asilimia kubwa timu hiyo bado inaendelea kuwatumia wachezaji wale wale ambao wengine wapo tangu 2017 na wanategemewa kuwa ni wa kikosi cha kwanza.

Na bahati mbaya sana wengine hawana hata wasaidizi ambao unaweza kusema wanaweza kukaa nje mechi mbili au tatu, timu ikacheza bila wasiwasi.

Ukweli usemwe tu kuwa viwango vya wachezaji wengi wa Simba hasa wale tegemeo au mgongo wa timu wenyewe, umri umewatupa mkono na wengine wamecheza mechi nyingi, hivyo wanahitaji mapumziko. Sasa wanapumzikaje wakati hao walioletwa ili wacheze viwango vyao haviaminiki kwa mashabiki mpaka kwa makocha wenyewe? Hili ni kosa la viongozi ambao walifanya kazi ya usajili.

Kengele ya hatari ambayo viongozi wake hawakuisikia, ilikuwa ni pale ilipotolewa dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botwana kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na kuangukia Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Ilifika robo fainali, lakini ukiiangalia ulikuwa unaona inaanza kupungua kasi na ubora wake. Ni kipindi kile ambacho viongozi wa Simba walitakiwa kufanya usajili mkubwa na si kuongeza wachezaji wa kuziba mapengo. Hata Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alikiri hivi majuzi kuwa baadhi ya wachezaji wamepungua viwango. "Simba imepungua ubora kidogo, lazima tuwe wa kweli. Kwanza kuna nyota wetu ambao ubora wao umepungua kidogo kwa sababu ya kuchoka, wamefanya kazi kubwa kwa miaka mitano, wamecheza sana kwa miaka yote hiyo michuano ya kimataifa, Ligi Kuu na michuano mingine mfululizo, hakuna binadamu ambaye anaweza kukupa asilimia 100 kwa miaka mitano, Mungu hajamuumba binadamu wa hivyo.

"Na unafahamu mpira ni kazi ya nguvu na kutumia akili na muda, unapocheza inatakiwa akili yako ifanye kazi kwa haraka sana, ukifanya kazi hiyo kwa miaka hiyo mfululizo lazima utachoka na kiwango kinapungua, ndiyo maana unaona ubora huo umepungua kwa sasa. "Kingine ambacho unaweza kuona ubora huo umepungua kidogo kwenye timu yetu, wapo watu wameondoka kwenye timu yetu, ama wameuzwa, au viwango vyao vilipungua, wakauzwa," alisema na kuongeza:

"Mohamed Hussein 'Tshabalala', anacheza hatua ya awali ya michuano ya kimataifa, hatua ya kwanza, mechi sita za makundi na robo fainali kwa miaka mitatu, usitegemee baada ya hapo atakuwa kwenye kiwango kile kile, ni lazima kiwango kitapungua kidogo." Kwa maneno haya tu, sidhani kama unaweza kumlaumu Robertinho kwa jinsi ambavyo timu kwa sasa inacheza, ikipata matokeo ya kusuasua.

Na kwa bahati mbaya sana kwa madirisha yote mawili ya usajili yaliyopita, Simba ilikuwa inasajili wachezaji bila kuwa na Kocha Mkuu. Watu walikuwa wanajisajilia bila malengo. Makosa makubwa ya Simba yapo kwenye usajili huku ikiendelea kusalia na kundi la wachezaji ambao viwango vyao vimepungua mno.

Si Robertinho tu, hata Zolan Maki, kocha aliyeondoka alikuwa analalamikiwa sana na mashabiki wa Simba kuwa timu haichezi vema na inapata matokeo ya kusuasua. Je, makocha wote wanaokuja Simba ni wabaya?

# Mil. 200/- zatolewa kwa vijana kuleta mabadiliko

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Marekani kwa kushirikiana na Zanzibar, imezindua mradi wa miaka minne kuwasaidia vijana wenye thamani ya dola milioni 10.6 (Sh. 247,934,000) ili wawe mawakala wa kuleta mabadiliko katika jamii zao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma na Ubalozi wa Marekani nchini, mradi huo unaojulikana kama Kijana Nahodha, unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), ukilenga kutoa ujuzi kwa vijana wa Kitanzania na kuwasaidia kuwa mawakala wa kuleta mabadiliko kwenye jamii zao.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa Kijana Nahodha utatekelezwa na asasi ya wazawa isiyo ya kiraia ya T-MARC kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Zanzibar (visiwani Unguja na Pemba).

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi ndiye aliyezindua mradi huo kwenye hafla iliyohudhuriwa na wajumbe wa wizara, wawakilishi wa kanda ya Zanzibar, mawakala wa serikali, mashirika ya kimataifa ya maendeleo, asasi za kiraia na vijana wa Zanzibar.

"USAID Kijana Nahodha ni mradi wa sekta mtambuka unaofanya kazi katika sekta ya ajira, elimu, kilimo, utawala bora na afya na unalenga kujenga uwezo wa vijana wenye umri kati ya miaka 15-25. Kujenga uwezo huu ni pamoja na kuongeza upatikanaji na ubora wa stadi mbalimbali.

"Unalenga kutoa mafunzo ya ufundi; kuboresha uelewa wa afya ya akili kupitia zana za elimu ya kidijitali zinazoongozwa na watu binafsi na kuimarisha njia za wazi za mawasiliano kati ya vijana na serikali za mitaa ili kuinua sauti za vijana katika maisha ya kiraia, siasa na utungaji sera," alisema.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mkazi wa USAID, Kate Somvongsiri alisema: "Kupitia Kijana Nahodha, tunalenga kuwawezesha vijana kupitia ujuzi mbalimbali; maarifa sahihi ya kuendesha biashara; msaada kutoka kwa familia zao, jamii, na serikali; ili wapate fursa kupitia elimu na ujuzi."

Mradi wa Kijana Nahodha unatarajiwa kuwawezesha vijana zaidi ya 45,000. Kati yao, takribani 10,000 kutoka Zanzibar na 35,000 mikoa miwili iliyolengwa ya Tanzania Bara.




Mkuu wa Mauzo wa Vodacom Tanzania PLC Kanda ya Kaskazini, George Venanty (katikati), akimjazia mteja mafuta kwenye Bajaj baada ya kulipia kupitia M-Pesa na kurejeshewa asilimia kumi ya pesa yake papo hapo mjini Moshi jana. Hii ni sehemu ya kampeni ya kampuni hiyo kupitia M-Pesa ya lipa kwa simu urejeshewe asilimia kumi ya pesa inayosisitiza malipo ya kidijitali ili kutunza hesabu, kuepuka upotevu na hatari zinazoambatana na ubebaji wa pesa taslimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafikishwa kortini kwa kushindwa kurejesha mikopo ya halmashauri

**Na Neema Hussein,** MPANDA

VIKUNDI 37 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi vimefikishwa mahakamani kwa kushindwa kurejesha Sh. milioni 61.5 ambazo ni fedha za mikopo itokanayo na asilimia 10 za mapato ya ndani ya halmashauri.

Kaimu Mkuu Idara ya Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Mpanda, Joshua Sankala alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati wa hafla ya kukabidhi mfano wa hundi ya mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu iliyotolewa na Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda.

Sankala alisema moja ya changamoto ni ufinyu wa bajeti kulinganisha na mahitaji, pia baadhi ya vikundi kutorejesha mikopo kwa wakati, akibainisha kuwa vikundi vinavyosumbua kurejesha ni vya vijana na watu wenye ulemavu.

"Utatuzi wa changamoto hizi ni kushirikiana na taasisi za kifedha ili watoe mikopo katika vikundi kwa riba nafuu na kuhakikisha wadaiwa wote wanalipa mikopo ili na wengine wakope kwa kuwapeleka mahakamani," alisema Sankala.

Kutokana na kusuasua kurejesha kwa mikopo hiyo, Mkuu wa wilaya ya Mpanda, Jamila Yusuph, aliiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuhakikisha inafuatilia fedha hizo zirudishwe ili kusaidia vikundi vingine.

"Kwenye taarifa inaonyesha kuna deni sugu la Sh. milioni 61.5, hawa wadaiwa sugu sio kwamba hawapo, wapo na kinachosababisha kupata wadaiwa sugu ni pamoja na vikundi kupoteza malengo, kwa mfano mmepanga mkitoka hapa mnakwenda kuanzisha labda kiwanda chenu cha kusindika alizeti, mkifika huko mnagawanyika. "Hili halikubaliki na hatutawaacha, ile dhana kwamba hizi fedha ni za serikali na unaweza ukafanya chochote na ukatoweka, hakuna kutoweka, utakapokuwapo tutakufuata. Kwa hiyo, TAKUKURU mfuatilie hizi fedha," aliagiza Jamila.


Kiongozi huyo pia aliwataka vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kutumia fursa ya mikopo hiyo vizuri.

Aliwaagiza maofisa maendeleo ya jamii kuanzia halmashauri hadi ngazi ya kata kushirikiana na madiwani kuwatafuta watu wenye ulemavu ili wapate haki yao ya kutumia mikopo hiyo ya asilimia 10 ambayo hugawanywa asilimia nne kwa wanawake, asilimia nne kwa vijana na asilimia mbili kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

"Suala lingine kwa vijana tuna historia mbaya, kijana aliyepewa mkopo wa bajaj, akaenda kuuza na ninyi vijana mliopo hapa mkipewa mkopo huu wengine bajaj, wengine pikipiki, marufuku kuuza, mkatumie kama mlivyoleta andiko lenu, mkifanya kinyume, mtachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria," alionya Jamila.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, Sophia Kumbuli, alisema wamelipokea agizo la kuwapata watu wenye ulemavu na tayari ofisi yake imeagiza wapatikane ili wapatiwe haki yao.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# TEF yahimiza mshikamano katika marekebisho ya Sheria ya Habari

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile amehimiza mshikamano miongoni mwa Watanzania pindi wanapojadili Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016.

Amesema pamoja na kwamba kila mtu ana mtazamo wake juu ya sheria hiyo, kinachotakiwa ni kuwa na umoja na mshikamano ili Tanzania ipate sheria nzuri inayosimamia sekta ya habari nchini.

Balile aliyasema hayo hivi karibuni alipozungumza katika kipindi cha Kipima Joto kinachorushwa na Kituo cha Runinga cha ITV.

Mbali na Balile, wengine walioshiriki mjadala huo uliokuwa na kichwa cha habari 'Muswada wa Sheria ya Habari Unaopendekezwa, una tija kwa wanahabari?' ni Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa

Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Joyce Shebe pamoja na Mjumbe wa Umoja wa Wadau wa Kupata Habari (CoRi), Deus Kibamba.

Balile alisema wakati mchakato wa kuandaa muswada huo ukiendelea, baadhi ya maofisa

wa serikali wanaohusika na masuala ya sheria, hawakutaka kutoa ushirikiano wala kusikiliza maoni ya waandishi wa habari

yaliyolenga kuboresha sheria hiyo kabla muswada haujawasilishwa katika Bunge la 10 lililoahirishwa mwishoni mwa mwezi Februari mwaka huu.

"Wakati tunafuatilia masuala ya muswada huu, kuna báadhi ya maofisa wa serikali walionekana kabisa kwamba hawataki mabadiliko yoyote katika sheria hiyo.

"Yaani, hao maofisa wa serikali wanajiona wao ni raia wa daraja la kwanza katika nchi hii kwani walikuwa wakikataa kila hoja tuliyokuwa tukiiwasilisha.

"Pamoja na hayo ambayo yameshapita, ninaomba mijadala juu ya sheria yetu hiyo, isijadiliwe kwa chuki, bali watu wavumiliane pindi panapotokea wengine wanaleta hoja ambazo wao hawazipendi kwani mijadala siku siku zote inaleta afya," alisema.

Balile pia alimpongeza Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape

Nnauye, kwa kile alichosema kwamba alijitahidi kufanikisha uwasilishwaji wa muswada huo bungeni.

"Hapo katikati kulitaka kutokea sintofahamu kati ya Nape na wanahabari hasa pale (Greson) Msigwa (Msemaji Mkuu wa Serikali), alipozungumza na wanahabari


na kusema muswada huo hautawasilishwa bungeni kama ilivyokuwa imeahidiwa na serikali.

"Pamoja na kuwapo hali hiyo, bado ninawaambia Waziri Nape amefanya kazi kubwa sana hadi kuhakikisha muswada unawasilishwa bungeni ukiwa na baadhi ya

maoni ya wadau katika baadhi ya vifungu ingawa baadhi ya vifungu tulivyokuwa tukilalamikia, havikufanyiwa marekebisho," alisema Balile.

Mwenyeti wa TAMWA, Joyce, alisema kuna haja Watanzania kuendelea kuujadili muswada huo kwa kuwa sheria itakayotungwa siyo ya wanahabari peke yao, bali ya Watanzania wote.

"Tayari muswada umesomwa kwa mara ya kwanza bungeni, sasa kinachotakiwa ni Watanzania wote kuendelea kuujadili kwa kina ili wabunge wapate fursa ya kutosha kwa ajili ya kutunga sheria nzuri kwa ajili ya Watanzania," alisema.



Meneja Mwandamizi (Rasilimali watu) wa GGML, Charles Masubi, akipokea tuzo kutoka kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## GGML yang'ara tuzo za ATE, Majaliwa aahidi makubwa

**Na Mwandishi Wetu**

JITIHADA za Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kuwajengea uwezo wahitimu wa vyuo vikuu kwa kuwapatia mafunzo kazini, zimeendelea kuonekana baada ya kampuni hiyo kuibuka mshindi wa pili katika tuzo zilizoandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET).

GGML imebeba tuzo katika kundi la waajiri wakubwa kutokana na mchango wake wa uzalishaji wa rasilimaliwatu wenye ubora kwa soko la ajira.

Hatua hiyo inakuja siku chache baada ya kampuni hiyo kupokea wahitimu 50 kutoka vyuo vikuu mbalimbali nchini ambao wameanza kupatiwa mafunzo kazini mwaka huu. Kati yao, 30 ni wanawake na 20 wanaume. Mwaka jana, jumla ya vijana 26 walihitimu mafunzi hayo ndani ya GGML.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hiyo katika hafla iliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Meneja Mwandamizi (Rasilimaliwatu) wa GGML, Charles Masubi, alishukuru serikali kwa kutambua mchango wa kampuni hiyo katika uzalishaji wa vijana bora wanaokubalika katika soko la ajira.

Awali Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, alisema serikali itaendelea kushirikiana kikamilifu na sekta binafsi katika utoaji elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kuzalisha wataalamu wenye ujuzi wa kutosha unaohitajika katika sekta mbalimbali.

Pia aliwapongeza waajiri kwa kutoa nafasi za mafunzo kwa vitendo, uanagenzi, utarajali pamoja na namna wanavyoshiriki katika kuandaa mitaala inayotumika kwenye vyuo na taasisi za elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

Alitoa wito kwa waajiri wote nchini kuendelea kushirikiana na serikali katika kuhakikisha malengo ya kukuza ujuzi na kuongeza soko la ajira yanafanikiwa kwa mustakabali wa maendeleo ya taifa.

"Maendeleo ya uchumi wa nchi yoyote yanategemea sana ngazi ya ujuzi wa nguvukazi uliyokuwa nayo. Hivyo, mchango wa wadau ni muhimu," alisema.

Aliongeza kuwa ushirikiano huo ni muhimu katika kuendeleza ujuzi kwa ajili ya kujenga uchumi wa viwanda.

"Ninataka nitumie fursa hii kuwapongeza lakini serikali inatambua na inathamini juhudi mnazozifanya katika utoaji wa ajira kwa wahitimu wetu, tunawapongeza sana," alisema.

Akizungumzia kuhusu kauli mbiu ya mwaka huu inayosema 'Kuimarisha Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa Uzalishaji wa Wafanyakazi Wenye Ujuzi Tanzania', Waziri Mkuu alisema ni thabiti kwa kuwa inaweka msisitizo katika ujenzi wa rasilimali watu yenye ujuzi.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uendelezaji wa Ujuzi wa Mwaka 2016/17-2025/26 ambao moja ya malengo yake ni kuwa na ushirikiano kati ya waajiri, wadau na vyuo au taasisi za elimu.

Mtendaji Mkuu wa ATE, Suzanne Ndomba-Doran, alisema ili Tanzania iweze kushiriki kikamilifu katika soko shindani la Afrika Mashariki na dunia, ni lazima hatua za makusudi zichukuliwe katika kukuza ujuzi hususani kwa vijana.

## Watatu wajitokeza kumrithi Mrema

**Na Sabato Kasika**

WANACHAMA watatu wa Chama cha Tanzania Labour Party (TLP), wamejitokeza kuchukua na kurejesha fomu za kuomba kuwania nafasi ya Uenyekiti wa Taifa wa chama hicho.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Katibu Mkuu wa TLP, Richard Lyimo, aliwataja wanachama hao kuwa ni Dominata Rwechungura, Ivan Maganga na Abdul Shangawe.

Katibu Mkuu huyo alisema chama hicho kinatarajiwa kufanya uchaguzi wa mwenyekiti wiki hii pamoja na wajumbe wawili wa Baraza la Wadhamini na Katibu Mipango.

"Hadi sasa ni wanachama hao watatu walioomba kuwania nafasi ya Mwenyekiti wa Taifa, inawezekana wakaongezeka wengine. Mwisho wa kurudisha fomu ni leo saa nane mchana," alisema Lyimo.

Alifafanua kuwa Baraza la Wadhamini la chama hicho linaundwa na wajumbe sita na kwamba wawili kati yao kwa sasa wanaumwa, hivyo nafasi zao zitajazwa na wengine katika uchaguzi huo.

"Lakini katibu mipango wa chama chetu anaumwa, hivyo tutachagua mwingine kuziba nafasi yake, ili shughuli za chama ziendelee kusonga mbele, ili kujiandaa kwa uchaguzi wa mwaka 2024/2025," alisema.

Alisema ni muhimu chama kipige hatua kwenda mbele na kwamba maandalizi ya kufanikisha uchaguzi huo utakaohudhuriwa na wajumbe 142 wa mkutano mkuu, yako katika hatua za mwisho.

"Bahati mbaya hatukualika vyama vingine vya siasa kuja kushuhudia uchaguzi, kutokana na sababu ambazo ziko juu ya uwezo wetu, lakini msajili wa vyama vya siasa kama mlezi vya vyama, amealikwa," alisema.

Nafasi ya Mwenyekiti wa TLP Taifa, ilikuwa ikikaimiwa na Hamad Mkadam aliyechaguliwa na sekretarieti ya chama hicho Septemba mwaka jana baada ya kifo cha aliyekuwa Mwenyekiti, Augustine Mrema aliyefariki dunia Agosti mwaka jana.



## Shule 16 Kilimanjaro zapokea msaada wa kompyuta

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

KAMPUNI ya Vodacom Tanzania imetoa msaada wa kompyuta katika shule 16 za Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro zikiwa na thamani ya Sh.milioni 115 ili kuwawezesha wanafunzi na walimu, kupata maudhui ya elimu ikiwamo vitabu vya kiada na ziada bila malipo yoyote.

Shule zilizonufaika na msaada huo ni pamoja na Kirongo, Mashati, Kwakoko, Mkuu, Tarakea, Nanjara, Mbomai, Umarini, Ndueni, Motamburu na Urauri.

Akizungumza jana katika Shule ya Sekondari Mrereni, wakati wa makabidhiano ya vifaa hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kisare Makori, aliishukuru Vodacom, kwa jitihada zake za kuhakikisha wanakuwa kinara wa utoaji wa elimu kwa njia ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Katika makabidhiano hayo ya baadhi ya vifaa, Mkuu wa Wilaya hiyo, aliwakilishwa na Ofisa Tarafa ya Vunjo Magharibi, Khamisuu Uledi.

"Elimu katika dunia ya sasa, imebadilika kwa kiasi kikubwa kutoka kutegemea walimu kuingia darasani na vitabu, mpaka shughuli zote kuhamia mtandaoni.

"Ningependa kuwapongeza Vodacom Tanzania, kwa kutoa msaada huu mkoani kwetu, ambao utakuwa msaada kwa walimu. Utawarahisishia utendaji wao wa kazi na hili litafanikiwa kwa kuwa tumepata vifaa vya kiteknolojia kama vile kompyuta hizi mlizozikabidhi leo (jana).

"Ningependa kutoa wito kwa shule ambazo zimekabidhiwa kompyuta hizi kuzitumia kwa matumizi yaliyokusudiwa ili kuendeleza kuboresha mfumo wa utoaji wa elimu nchini. Bila shaka zitakuwa chachu kwa walimu kusaidia ufanisi katika ufundishaji wao."

Vodacom, imekabidhi kompyuta 10 kwa shule tano, ambazo ni Shule ya Sekondari Marlex, Sakayo, Mrereni, Mangoto na Mwika.

Akielezea malengo ya kukabidhi vifaa hivyo, Mkuu wa Kanda ya Kaskazini, Vodacom Tanzania PLC, George Venanty, alisema: "Ni fahari kwetu kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali katika upatikanaji wa elimu bora nchini kwa kuwawezesha walimu na wanafunzi kujipatia vitabu bila ya malipo kwa njia ya mtandao."

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Mrereni, Mary Masuki, aliishukuru Kampuni ya Vodacom, kwa kutekeleza kwa vitendo adhma yake ya kuwa kampuni inayoongoza kwa mawasiliano ya kiteknolojia na dijitali nchini huku ikizinufaisha jamii za Watanzania kwenye nyanja mbalimbali za kimaendeleo.

Programu ya bure ya e-Fahamu, ilianzishwa na Vodacom Foundation mwaka 2017 ili kuwasaidia walimu na wanafunzi kupata vitabu vya ziada na kiada kwa shule za msingi na sekondari.

Mwaka 2022, Vodacom Tanzania PLC, kwa kushirikiana na Taasisi ya African Child Projects (ACP), walizindua rasmi upanuzi wa mradi wa uunganishwaji wa shule kidijitali, mradi uliolenga kuunganisha shule kadhaa nchini kwenye mtandao wa intaneti.

# Wahukumiwa jela maisha kwa kumbaka mwanafunzi

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

WAKAZI watatu wa Kijiji cha Karansi, Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, wamehukumiwa kifungo cha maisha jela baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kumbaka, kumwingilia kinyume na maumbile mwanafunzi wa shule ya msingi iliyoko kijijini humo mwenye umri wa miaka 12.

Waliohukumiwa adhabu hiyo na Mahakama ya Wilaya ya Siha ni Fredrick Mollel (29), Degratus Fredrick (26), ambaye ni mfanyabiashara pamoja na mama mzazi wa mwanafunzi huyo Maria Laizer (35).

Akisoma hukumu hiyo, mwishoni mwa wiki, Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Elibahati Petroi, alisema washtakiwa hao wametiwa hatiani baada ya mahakama hiyo kuridhika na namna upande wa mashtaka ulivyoijenga kesi hiyo.

Alisema ushahidi uliotolewa na mashahidi wa upande wa mashtaka akiwamo daktari aliyefanya uchunguzi wa kitabibu, mwalimu anaposoma mwanafunzi huyo pamoja na mwathirika mwenyewe, mahakama imejiridhisha pasipo shaka kwamba washtakiwa hao walitenda kosa hilo.

Katika hukumu hiyo, Hakimu Petroi, alisema washtakiwa hao walitenda kosa hilo Septemba 19, mwaka jana, majira ya saa 3:00 usiku nyumbani kwa mama mzazi wa mwanafunzi huyo akiwa amelala.

Hakimu huyo alisema mwanafunzi huyo akiwa amelala, mama yeke alimfuata chumbani akiwa ameongozana na washtakiwa wawili wanaume, mama yake alimuamsha na kumwambia avue nguo na kumlazimisha kufanya mapenzi na watu hao kwa ujira wa Sh. 5,000.

Kwa mujibu wa Hakimu Petroi, washtakiwa hao walifanya kosa hilo kinyume na Kifungu 131 a (1) (2) (3) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2022 na ni kinyume na Kifungu 154 (1) cha Sheria hiyo.

Awali, ilidaiwa mahakamani humo na Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Kurwa Mungo, kuwa wakati ukatili huo ukiendelea mama mzazi alimziba mdomo mtoto wake ili kelele zisisikike.

Iliendelea kudaiwa kuwa baada ya kutekeleza ukatili huo mama mzazi akiwa anashuhudia washtakiwa hao walitokomea na kumuacha mwanafunzi huyo akiugulia maumivu kutokana na majeraha aliyoyapata.

Aidha, inaelezwa kuwa siku iliyofuata mwanafunzi huyo alipofika shuleni alimpa taarifa mwalimu wake, ambaye alichukua jukumu la kutoa taarifa Kituo Kikuu cha Polisi Sanya Juu na washtakiwa walitiwa nguvuni.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, mwendesha mashtaka huyo aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali dhidi ya washtakiwa kutokana na kitendo kilichofanyika ni cha kinyama, ambacho mama mzazi alishiriki.



Mratibu Lishe Shuleni wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mwalimu Grace Shileringo, akizungumza na maofisa wanaotekeleza programu jumuishi ya taifa ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto (PJT-MMMAM) mkoani Manyara juzi pamoja wadau wa maendeleo wanaotekeleza mradi wa mtoto kwanza, (wa pili kulia) ni Ofisa Elimu Manyara, Halfani Masukira. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Shule zaagizwa kuanzisha mashamba kupambana na udumavu

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeagiza shule zote za Mkoa wa Manyara kuanzisha mashamba kwa ajili ya kuzalisha chakula kitakachotumika na wanafunzi ili kupambana na tatizo la udumavu linaoutesa mkoa huo.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mratibu wa Lishe Shuleni wa Wizara hiyo, Grace Shileringo, wakati wa kikao kazi cha robo ya pili ya mapitio ya utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM).

Mratibu huyo alisema ni vizuri suala la lishe wataalamu wakatumia mwongozo wa lishe shuleni uliopo ili kuhamasisha kupatikana kwa chakula na kuwanusuru wanafunzi wanaoshinda na njaa.

"Mashamba ya shule yatumike kuzalisha chakula cha wanafunzi. Tunataka kuanzia sasa wanafunzi walime mboga, matunda na mazao mengine ya nafaka, ambayo watakula wao wenyewe na kuepuka tatizo hili la udumavu," alisema Shileringo.

Aidha, aliagiza walimu wa awali, kuwa na madarasa yanayozungumza ambayo yana kona nne za ujifunzaji wa awali ili kumsaidia mwanafunzi asome kwa vitendo na picha zenye mpangilio.


Vilevile, aliagiza halmashauri zote mkoa huo kuanza kutenga bajeti ya PJT-MMMAM ili kurahisisha utekelezaji wa programu hiyo na kuwapunguzia mzigo wadau wa maendeleo ambao wanasaidia utekelezaji wake.

Kabla ya agizo hilo, Ofisa Elimu wa Mkoa wa Manyara, Halfan Masukira, alisema mkoa huo una shule 699, ambazo zote zinatoa chakula shuleni.

Kuhusu PJT-MMMAM, Masukira, aliwaomba wataalamu wa ngazi zote na wadau kutoa elimu juu ya programu hiyo kila kona, kwa kutumia lugha rahisi kufikisha ujumbe.

Ofisa Mradi wa Mtoto Kwanza kutoka Shirika la Tanzania Early Children Development Network (TECDEN), Christopher Peter, aliupongeza Mkoa wa Manyara, kwa kutoa chakula kwa wanafunzi.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa PJT-MMMAM, kuanzia Oktoba hadi Desemba mwaka jana, Kaimu Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, Dickson Maramoko, alisema shule 89 za serikali zimeanzisha madarasa ya awali, ambapo shule tano ni za binafsi.





# H'shauri yatenga mil.360/- kuwapa wajasiriamali

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Ushetu mkoani Shinyanga imetenga Sh. milioni 361 kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya wajasiriamali katika mwaka wa fedha 2023/2024 utakaowawezesha kukuza mitaji yao na kujikwamua kiuchumi.

Fedha hizo zimetokana na makusanyo ya ndani, kwamba watapatiwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Hayo yalibainishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu, Afya na Maji wa Halmashauri hiyo, Kurwa Shoto wakati akijibu swali la Diwani wa Bulungwa, Ester Matone, aliyetaka kujua idadi ya vikundi vilivyopatiwa mikopo na kiasi gani kimetolewa.

Alisema, katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023 vikundi tisa vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vilipata mikopo ya Sh. milioni 219.8 kutoka kata nane kati ya 20 zilizoko ambazo wameanza kuzitumia katika utekelezaji wa kukuza mitaji yao na kuongeza kipato cha kaya.

Alieleza kuwa kikundi cha wanawake Kata ya Mpunze kilipata Sh.milioni 100, Kata ya Chambo Sh.milioni 12, Nyamilangano Sh. milioni 15, Kinamapula Sh.milioni 12, Ulowa vijana Sh.milioni 20.8, Ushetu wanawake Sh.milioni 10 na Ukune kikundi cha watu wenye ulemavu Sh.milioni tatu.

Diwani wa Nyamilangano, Robert Mihayo aliwasihi maofisa maendeleo ya jamii kwa ngazi za kata kutoa elimu ya usimamizi wa fedha kwa vikundi vinavyopatiwa mikopo hiyo ili viweze kujiendesha kibiashara.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri Morgani, Mwita, alisema kabla ya kuvipatia mikopo vikundi vya ujasiriamali huwa wanavitembelea na kukagua shughuli wanazozifanya na kuwapatia ushauri wa namna ya kufanya biashara na walezi wa vikundi hivyo ni maofisa maendeleo wa kata husika.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Gagi Lala alisema, wataendelea kutoa mikopo kwa vikundi vitakavyorejesha mikopo kwa wakati na kuwataka madiwani kuvisimamia vikundi hivyo ili viweze kujiendesha kibiashara na vile vitakavyoshindwa kurejesha vitawajibishwa kisheria kwasababu fedha za umma huwa haipotei.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Deus Kakulima, alisema wataendelea kutekeleza agizo la serikali la kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupitia fedha za mapato ya ndani na kuwataka waliokopeshwa kuhakikisha wanarejesha mikopo hiyo kwa wakati ili kuvipatia fursa vikundi vingine kukopa.

## Wanafunzi wapewa elimu utunzaji miundombinu ya maji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Town iliyoko Manispaa ya Shinyanga wameanza kupatiwa elimu na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA) juu ya utunzaji wa miundombinu ya maji ili wawe mabalozi katika kaya zao.

Elimu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki shuleni hapo na maofisa kutoka SHUWASA ikiwa ni mwendelezo wa kudhibiti uharibifu wa miundombinu hiyo sambamba na kuitunza ili iendelee kutoa huduma.

Ofisa kutoka Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano SHUWASA, Monica Ndeha, alisema wametoa elimu hiyo kwa wanafunzi ili wakaisambaze majumbani mwao, kwenda kuzungumza na wazazi juu ya huduma za maji ambazo hutolewa na mamlaka hiyo ikiwa ni pamoja na kutunza vyanzo vya maji na miundombinu ya mabomba.

Naye Msaidizi wa Ofisa Dira na Ankara kutoka SHUWASA, Justine Mbijuye, aliwataka wanafunzi wanapokuwa shuleni au nyumbani kutumia maji vizuri na kutokuwa na tabia ya kuyamwaga ovyo na kusababisha kwani hatua hiyo husababisha ankara za maji kuja kubwa na kuziingizia hasara taasisi na familia zao.



Ofisa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), Monica Ndeha, akitoa elimu kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Town Manispaa ya Shinyanga kuwa mabalozi wazuri wa kutunza miundombinu ya miradi ya maji na vyanzo vyake, hasa utoaji taarifa wanapoona mabomba yamepasuka ili kuzuia upotevu wa maji. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wahukumiwa jela maisha kwa udhalilishaji kijinsia

**Na Halima Ikunji,** TABORA

JESHI la Polisi mkoani Tabora limesema katika kukabiliana na kudhibiti makosa ya ukatili wa kijinsia wamewafikisha mahakamani watuhumiwa wawili na kuhukumiwa kifungo cha maisha jela.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Richard Abwao, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alisema kuwa Februari 2, mwaka huu, Mahakama ya Mkoa wa Tabora ilimuhukumu Mussa Mohamedi (18) na mkazi wa Malolo Manispaa ya Tabora kifungo cha maisha jela baada ya kupatikana na hatia katika kosa la kulawiti mtoto mwenye umri wa miaka mitano.

Aliongeza kuwa Februari 17, mwaka huu Mahakama ya Wilaya ya Nzega ilimuhukumu Shabani Kichwa (19) kifungo cha maisha jela baada ya kukutwa na hatia katika kosa la ubakaji. Vilevile alisema kuwa Mahakama ya Wilaya ya Nzega mkoani hapa iliwahukumu mke na mume ambao ni Magina Kulwa na Zainabu Yahaya kifungu cha mwaka moja jela baada ya kupatikana na hatia ya kumwozesha mwanafunzi wa darasa la nne na kumwachisha masomo yake.

Mwanafunzi huyo aliyekuwa akisoma Shule ya Msingi Mwanzoli iliyopo wilayani Nzega mkoani hapo ambapo licha ya kutoa hukumu hiyo kwa mke na mume pia mahakama hiyo ilitoa hukuma kwa watu wengine 10 wote wakiwa ni wakazi Kijiji cha Mwanzo, Kata ya Igusule, Tarafa ya Mwakalundi wilayani humo.

Kamanda Abwao alisema Jeshi la Polisi linaendelea na operesheni mbalimbali kwa ajili ya kukomesha vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Nipashe Spotika



KLABU ZENYE MASHABIKI 'VICHAA' ZAIDI DUNIANI 12 - 13




MESSI

# WACHEZAJI WA5 AMBAO MARA CHACHE HUTUMIA MGUU DHAIFU

**LONDON, England**

INGAWA wachezaji wengi wamefunzwa kutumia miguu yote kwa usawa, wengine wanaweza kuwa na upendeleo wa asili kwa mguu mmoja juu ya mwingine. Katika soka, wachezaji huwa na mguu unaotawala au wanaopendelea ambao hutumia kwa udhibiti mkubwa, usahihi na nguvu.

Hata hivyo, inaweza pia kuwa hasara ikiwa timu pinzani inafahamu udhaifu wa mchezaji na inaweza kumdhibiti kwa ulinzi ipasavyo.

Kumekuwa na wachezaji wengi wenye mafanikio wa mguu mmoja katika historia ya soka, kama vile Diego Maradona, ambaye anachukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji bora wa wakati wote, licha ya kutumia mguu wa kushoto pekee.

Acha sasa tuangalie wachezaji watano wa kiwango cha dunia ambao huwa wanatumia mara chache zaidi miguu yao dhaifu...

**#5 Bernardo Silva (Manchester City)**

Bernardo Silva ni kiungo mshambuliaji mahiri anayejulikana kwa wepesi wake na ubunifu. Ni mwanasoka mwenye kipaji cha kiufundi ambaye anastareheshwa na mpira miguuni mwake na ana ujuzi bora wa kudhibiti.

Silva pia anafahamika kwa ukimbiaji wake wa akili na uwezo wa kutengeneza nafasi za kufunga kwa wachezaji wenzake pamoja na pasi zake sahihi. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno ni mchezaji mwenye juhudi ambaye huchangia katika safu ya ulinzi na ushambuliaji, na kumfanya kuwa mtu muhimu kwa timu yoyote.

Silva ni mchezaji anayetumia mguu wa kushoto na ni nadra kumuona akijaribu kupiga shuti au hata pasi kwa kutumia mguu wake wa kulia. Licha ya hayo, anaendelea kuwa mmoja wa viungo wabunifu kwenye Ligi Kuu England.

**#4 Angel Di Maria (Juventus)**

Angel Di Maria ni winga anayetumia mguu wa kushoto ambaye anafahamika kwa ubora wake wa kipekee na uwezo wa kucheza chenga. Kwa kiasi kikubwa ni mchezaji mwenye mguu mmoja, anayetegemea sana mguu wake wa kushoto kudhibiti, kutoa pasi na kupiga mpira.

Licha ya hayo, Di Maria amekuwa na mafanikio katika kiwango cha juu zaidi cha soka na anachukuliwa kuwa mmoja wa mawinga bora wa kizazi chake.

Anafidia uchezaji wake wa mguu mmoja kwa kasi, wepesi na maono, jambo ambalo linamfanya kuwa mchezaji mgumu kwa mabeki kumzuia. Uwezo wa Di Maria kuwapiga mabeki na kutoa krosi hatari kwa mguu wake wa kushoto umekuwa jambo muhimu katika mafanikio yake katika maisha yake yote ya soka.

Kwa sasa, akiwa Juventus, nyota huyo wa Argentina amepita kiwango chake, lakini alichangia kwa kiasi kikubwa katika ushindi wa La Albiceleste kwenye Kombe la Dunia mwaka jana nchini Qatar, hata kufunga bao katika fainali dhidi ya Ufaransa.

**#3 Kyle Walker (Manchester City)**

Kyle Walker ni beki wa pembeni wa kisasa ambaye anafanya vema katika safu ya ulinzi. Ana kasi ya kipekee, inayomfanya kuwa mali muhimu, haswa wakati wa mabadiliko ya ulinzi. Walker pia anajulikana kwa krosi zake sahihi na kukimbia kwa kupishana, ambayo hutoa tishio la ziada la mashambulizi kwa timu yake.

Walker mara nyingi huwa na mguu wa kulia. Yeye si maskini na mguu wake dhaifu, lakini ni nadra kumuona akiutumia. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, kwa kawaida huwekwa kwenye ubavu wa kulia na kwa hiyo, hajawahi kuhitajika kutumia mguu wake wa kushoto.

**#2 Paulo Dybala (AS Roma)**

Paulo Dybala aliondoka Juventus na kujiunga na AS Roma kama mchezaji huru msimu uliopita. Ni hatua ambayo imefanya maajabu kwa mshambuliaji huyo wa Argentina kwani ameweka kiwango chake katika Uwanja wa Olimpico.

Dybala amekuwa mchezaji bora wa Roma hadi sasa msimu huu, akifunga mabao 11 na kutoa asisti saba katika mechi 22 za mashindano yote akiwa na 'Giallorossi' hao. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, ana nguvu kwenye mguu wake wa kushoto tu.

Lakini Dybala ana uwezo wa kukwepa upungufu huo kutokana na sifa zake za kiufundi na ubunifu kwenye medani ya soka.

**#1 Lionel Messi (Paris Saint-Germain)**


Lionel Messi anachukuliwa kuwa mmoja wa wanasoka bora wa wakati wote. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, ni mmoja wa washambuliaji waliojipanga vema katika historia ya mchezo huo na ameshinda takriban mataji yote makubwa aliyowahi kuwania.

Hivi majuzi zaidi, Messi aliivusha Argentina na kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia na kutwaa Mpira wa Dhahabu uliotolewa kwa mchezaji bora wa michuano hiyo. Mshindi huyo mara saba wa tuzo ya Ballon d'Or ni mchezaji anayetumia mguu wa kushoto na ingawa anafahamu vizuri mguu wake dhaifu, huwa anautumia mara chache sana.

Messi ameridhika kufanya yote kwa mguu wake wa kushoto, akiwapiga chenga wapinzani na kutengeneza nafasi. Ameonyesha kwamba kutumia miguu yote miwili si lazima.

## ISIKUPITE

HAT-TRICK Cristiano Ronaldo aliyofunga juzi Ligi Kuu Saudi Arabia dhidi ya Damac, ni ya pili kwake kwenye ligi hiyo, lakini inamfanya kufikisha mabao nane katika mechi tano alizoichezea Al-Nassr hadi sasa, akiwa amehusika kwenye mabao 10 baada ya kutupia nane na kutoa 'assists' mbili. Hivyo zinamfanya kuwa katika mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu. Kinara wa mabao hadi sasa kwenye ligi hiyo amecheka na nyavu mara 13.



## Extra Time




# KLABU ZENYE MASHABIKI 'VICHAA' ZAIDI DUNIANI

**LONDON,** England

UKIWA ndio mchezo maarufu zaidi duniani, mashabiki wa soka wameanzisha utamaduni wa kuunga mkono wachezaji wao, makocha, klabu na vitu vyote vinavyohusiana na timu zao.

Hapo awali, sehemu ya mashabiki wa klabu ambao walihudhuria michezo yake kwa tiketi za kila wiki zilizonunuliwa kutoka sehemu kubwa ambayo ipo jirani na mchezo huo unapofanyika.

Kwa mapinduzi ambayo televisheni ya satelaiti imeleta katika michezo, sasa klabu zina njia ya kupanua ufikiaji wao katika njia na masoko mengine na kusababisha umaarufu wa mchezo wa soka kusambaa katika maeneo mbalimbali duniani ambayo hapo awali yalikuwa yamelala kama vile nchi za ndani za Afrika, Asia na Oceania.

Makala haya inaziangalia klabu 10 zenye mashabiki bora zaidi 'vichaa' wa timu zao, twende sasa...

**#10 Bayern Munich**

Ikiwa ndio klabu Kuu ya Ujerumani na katika soka la Ulaya imekuwa ikipanua wigo wa mashabiki wake kila siku. Bayern Munich, ingawa mwanzoni haikuwa timu inayopendwa zaidi na Ujerumani, imepanda polepole hadi kufikia hadhi ya juu na raia wengi wa nchi hiyo.

Klabu hiyo imewekeza uwanjani na kucheza kwa uaminifu, uthabiti na kukua kwa kiwango kizuri. Wakati huo huo, timu yao ya uuzaji inawawezesha kushirikiana na mamilioni ya mashabiki kutoka masoko ambayo hayajatumiwa kama vile India, Mashariki ya Mbali, Uarabuni, Afrika na Australia.

Allianz Arena inaripoti wastani wa mahudhurio ya mashabiki 71,000 kwa mchezo, ambayo inashika nafasi ya nne kwa ukubwa wa sauti barani Ulaya na ya pili kwa ubora nchini Ujerumani (nyuma ya Borussia Dortmund). Idadi hii ni karibu asilimia 90 ya uwezo kamili wa mashabiki wote 80,000 (ambayo pia wanaruhusiwa kusimama, ambapo inaruhusiwa katika Ligi Kuu Ujerumani maarufu Bundesliga).

**#9 River Plate & Boca Juniors**

Ingawa klabu hizi hazijulikani sana nje ya eneo la soka la Amerika Kusini, watu wa hali ya juu wanaoshabikia klabu zote mbili wamezifanya kuwa maarufu kwa ushujaa wao, uanaharakati na usaidizi wa ukichaa kutoka kwa mashabiki wao. Dabi ya Jiji la Buenos Aires ni kati ya mechi yenye vurugu zaidi katika michezo yote na ina historia ya vurugu kutoka pande zote mbili.

Pamoja na ufikiaji wa mtandao kuingia katika masoko mapya, klabu zote mbili zinaanzisha polepole msingi wa kimataifa wa mashabiki. Wafuasi wao humiminika kwenye viwanja vilivyojaa msongamano kwa ajili ya michezo yao yote ya nyumbani na kufanya maisha kuwa magumu kwa timu yoyote inayowatembelea.

Uwanja wa Monumental ambao umekuwa wa nyumbani wa River Plate kwa kipindi cha miaka 78 sasa, una wastani wa idadi ya kuchukua mashabiki 70,000 kwa michezo yake. Boca wanatumia uwanja mdogo ulioundwa vizuri zaidi wa La Bombonera una wastani wa mahudhurio ya karibu mashabiki 50,000 kwa michezo ya ligi.

**#8 Lech Poznan**

Kwa watazamaji wa Ligi Kuu England, kumekuwa na madai kutoka klabu hii kwamba wao ndio waanzilishi wa staili ya kushangilia maarufu ya Manchester City ya sasa ya 'The Poznan' - inayoimbwa wakati wowote timu inapofunga bao. Ikizingatiwa kama klabu iliyofanikiwa zaidi katika historia ya Poland, wao hucheza mara kwa mara mbele ya watu zaidi ya 40,000.

Ingawa utukufu barani Ulaya umekuwa mgumu sana kupatikana kwa timu dhaifu ikilinganishwa na moja ya ligi dhaifu za bara, wafuasi wa Poznan, kwa muda mrefu, wamekuwa na msimamo wao kama mashabiki wa kweli kwa klabu yao.

Zaidi ya nusu ya wakazi wa nchi hiyo kutoka kizazi chake cha zamani bado wanaiunga mkono klabu hiyo, na maendeleo ya hivi majuzi katika ushirikishwaji wa mitandao ya kijamii yamewapa umakini mkubwa kama moja ya vituo vikuu vya ushabiki wa soka nchini humo.

**#7 Napoli**

Kwa kuwa hapo awali ilikuwa na fursa ya kuchezewa na gwiji wa Argentina, Diego Maradona, ushujaa mkubwa katika ngazi ya klabu, klabu hiyo inajulikana kwa kuwa na moja ya mahudhurio ya wastani wa juu zaidi barani Ulaya.

Uwanja wa San Paolo (ambao sasa unaitwa Diego Maradona) una uwezo wa kuchukua mashabiki 60,000 na mara zote hujaa, na ushiriki wao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa miaka mitano iliyopita umewapa sifa ya kimataifa na msingi wa kujionyesha kwa idadi kubwa ya wafuasi wa soka.

Napoli wana mashabiki wengi wa Italia, ambao wameamua mbinu mbalimbali ili kuanzisha kiwango cha mapenzi yao kwa klabu.

**#6 Roma & Lazio**

Uwanja wa Olympiastadion ni mwenyeji wa klabu hizi mbili zote za Italia.

Mashabiki wa Italia, kwa muda mrefu, wameweka kiwango cha wafuasi kutoka klabu zao na misingi ya mashabiki wa Roma na Lazio yenye makao yake jijini Rome ni makundi maarufu zaidi ya mashabiki kutoka nchi hii.

Wakiungwa mkono na CUCS (Commando Ultra Curva Sud), mashabiki wa Roma wanachukuliwa kuwa wa kihistoria zaidi katika soka la Ulaya. Ushindani wa klabu na Lazio unachochea moja ya dabi kali zaidi duniani.

Wachezaji wa hali ya juu wa Lazio pia wanashauku na historia ya mashindano ya klabu hizi mbili hufanya zinapokutana kuwa na ushindani mkubwa sana.

**#5 Celtic**

Katika moja ya mechi kati ya Celtic na wababe wa Ulaya, Barcelona kwenye Uwanja wa Celtic Park, ambao walishinda 2-1, Lionel Messi alinukuliwa akisema hivi: "Nimebahatika kucheza katika viwanja vikubwa barani Ulaya nikiwa na Barcelona, lakini hakuna hata mmoja wa kuulinganisha na Celtic."

"Mazingira ya mashabiki wao yanakufanya kuwa na usiku wa kipekee sana wa soka barani Ulaya."

**#4 Galatasaray**

Kura nyingi za mtandaoni zimefichua kuwa idadi kubwa ya mashabiki wa soka wa Uturuki wanaaminika kuunga mkono upande maarufu zaidi wa nchi hiyo, unaojulikana kwa kuunda mazingira ya uhasama na ya kutisha kwa timu zinazozuru.

Ryan Giggs alikuwa na haya ya kusema kutokana na mchezo wao wa ugenini kwenye Uwanja wa Turk Telekom Arena akiwa na Manchester United: "Sijawahi kukutana na kitu kama Galatasaray. Saa mbili kabla ya mechi kuanza, tulitoka kutazama uwanja, na uwanja ulikuwa umejaa tele!"

Mashabiki wao huwa wanazidi kupita kiwango, mara kadhaa katika mchezo wa ligi, wakirusha milipuko na vitu vingine mbalimbali chini wakati wa mchezo. Bado, kiwango chao cha mapenzi ni cha juu mno.

**#3 Manchester United**

Old Trafford imekuwa na sifa ya kuwa uwanja wenye sauti kubwa zaidi kwenye Ligi Kuu England kwa muda mrefu.

Nyakati nzuri za Old Trafford hazikuwa zimeisha kabisa, kwani hali ya joto kwenye uwanja imeathiri wazi timu nyingi zinazosafiri na kufanya maisha yao kuwa magumu katika historia ya soka nchini England. Uwanja huo ndio sehemu muhimu zaidi ya urithi wa United na una sanamu ya Sir Alex Ferguson, kocha aliyeipa mafanikio makubwa zaidi klabu hiyo.

United inajivunia kuwa pengine chapa kubwa zaidi katika soka na ni mojawapo ya klabu kubwa tatu duniani zenye mashabiki wengi mno kwenye mitandao ya kijamii (nyingine mbili zikiwa Real Madrid na Barcelona).

**#2 Liverpool**

Fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2005, ulikuwa usiku bora zaidi wa Ulaya kwa mashabiki wa Liverpool na walihakikisha muhuri wao unasikika kwenye mchezo huo, huku wakiendelea kuishangilia timu yao ambayo ilikuwa nyuma kwa mabao matatu dhidi ya AC Milan.

Usaidizi huo hakika ulikuwa na jukumu katika kusaidia Liverpool kuibuka tena kwenye mchezo na hatimaye ushindi wao wa mikwaju ya penalti.

Mashabiki wa Liverpool wameenea kote ulimwenguni na wanajivunia sana kuonyesha hadharani mapenzi yao. Wimbo wa 'You Will Never Walk Alone' huimbwa na usaidizi wa kusafiri katika kila Ligi Kuu na pia katika kila mchezo wanaocheza nje ya England. Hata katika msimu, katika maeneo ya mbali kama Melbourne, Australia, wimbo huu huimbwa na wafuasi wao washupavu.

**#1 Borussia Dortmund**

Kwa jiji lililo na idadi ya watu karibu 450,000 wote wanatajwa kuwa ni mashabiki wa klabu yao ya Borussia Dortmund.

Hii yenyewe, inaonyesha kiwango cha juu sana cha upendo wa ndani kwa klabu kwa mashabiki hao ambao wengi wao husafiri na timu hiyo kila sehemu.

Mashabiki wa Dortmund pia wanasifika kwa uungwaji mkono wao wa hali ya juu wakiwa safarini, kwani 20,000 kati yao walisafiri kila sehemu.


Uwanja wa Westfalonstadion, ambao sasa unaitwa Signal Iduna Park, unashuhudia wastani wa Watazamaji zaidi ya 80,000 katika kila mchezo, ambao mara kwa mara ni miongoni mwa takwimu za juu zaidi barani Ulaya. Wao ni wafuasi wazuri, wenye tabia njema, ambao hufaulu kuanzisha uhusiano na maeneo hata katika mchezo wa kusafiri.

## Nukuu

"Ninahisi kuzoea timu zaidi. Si rahisi kuzoea katika mechi tano, sita au saba; kila mtu anajua mikimbio yangu. Lakini naanza kuelewa mikimbio yao na wanaanza kuelewa mikimbio yangu, hatua kwa hatua, tunaweza kufikia kiwango kikubwa," **Nyota wa Al-Nassr, Cristiano Ronaldo, baada ya kufunga hat-trick ya pili juzi wakati timu yake ikiibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Damac kwenye mechi ya Ligi Kuu Saudi Arabia.**



"Kwa masikitiko makubwa, ni mwisho wa safari ambayo nilitarajia ingekuwa ndefu zaidi na ambayo ingemalizika kwa ladha nzuri kinywani, juu ya mafanikio yote tuliyopata na Wekundu wetu. Kwa unyenyekevu, nadhani kazi hiyo ilistahili kumalizika kwa sababu ya uamuzi wa kibinafsi au kwa sababu ya kiwango changu haukuwa kulingana na kile timu yetu ya taifa inastahili, lakini si kwa sababu ya umri au sababu nyingine bila kuzisikia," **Beki wa kati PSG, Sergio Ramos, akitangaza kutundika daluga Timu ya Taifa ya Hispania.**



"Kuna wachezaji wengi wazuri na Kylian ni mmoja wao. Ana nguvu sana! Wafaransa wana bahati sana kwamba anaichezea Ufaransa. Ningependa aicheze Norway ni wazi, lakini sivyo. Lakini ndio, yuko mchezaji wa ajabu. Ana kasi sana, ana nguvu sana na amekuwa akifanya hivyo kwa miaka mingi. Yeye ni nini? Ananizidi miaka miwili? Ni kichaa! Wakati mwingine lazima ujiambie kwamba bado ana miaka 10 ya kucheza kwenye kiwango cha juu ni jambo la ajabu," **Straika wa Manchester City, Erling Haaland, akimwelezea nyota wa PSG, Kylian Mbappe ambaye wanawekwa daraja moja la kushindana kama ilivyo kwa Lionel Messi na Cristiano Ronaldo.**



# UGUMU, URAHISI MECHI ZA UBINGWA YANGA LIGI KUU




**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi Yanga wamebakisha pointi 14 tu kuweza kutwaa Ubingwa wa Tanzania Bara kwa mara ya pili mfululizo. Ni kama vile tayari Yanga imeshaingia kwenye sebule ya chumba kilichohifadhiwa kombe hilo.

Yanga ambayo mpinzania wake halisi kwenye mbio za ubingwa ni Simba, inahitaji ushindi kwenye mechi tano kati ya saba zilizobaki ili kuwa mabingwa wa Tanzania.

Kwa sasa Yanga imefikisha pointi 62, hivyo kama itacheza mechi tano na kushinda, itazoa pointi 15 na kufikisha jumla ya alama 77 ambazo hazitofikiwa na timu yoyote ikiwamo Simba.

Simba ambayo ina pointi 54 na imebakisha mechi saba ili imalize mechi zake zote 30 msimu huu, kama itashinda zote inazoa jumla ya pointi 21 ambazo ukizijumlisha na 54 ilizonazo unapata pointi 75, ambazo hazitoweza kuizuia Yanga kutwaa ubingwa.

Kimahesabu ni kwamba pointi 14 tu za Yanga zinatosha kuipa ubingwa kwani ukijumlisha na 62 ilizonazo unapata pointi 76, moja zaidi ya ambazo Simba itavuna ikishinda mechi zote.

Kwa takwimu na hesabu zote hizo, inaonyesha Yanga iko karibuni zaidi na ubingwa. Kitu pekee ambacho kinaweza kuchelewesha ubingwa huo ni kwamba kati ya mechi hizo tano ilizosalia, itacheza dhidi ya Simba inayoifukuza, mchezo unaotarajiwa kupigwa Aprili 6, mwaka huu.

Iwapo itashinda basi hesabu hizo zinaweza kutimia kwa asilimia 100, lakini kama itafungwa au kutoka sare, inabidi idadi inayotakiwa ya pointi itafutwe kwenye mechi zingine.

Hata hivyo, pamoja na mahesabu yote, lakini itategemea pia na matokeo ya mechi za Simba, ambapo kama kati ya hizo saba baadhi itapoteza au kutoa sare, itairahisishia njia zaidi Yanga.

Zifuatazo ni mechi tano ambazo kama ikichanga katara zake vizuri, basi itatawazwa kuwa mabingwa msimu wa 2022/23.

**1. Yanga vs Geita Gold**

Mechi hii imepangwa kuchezwa Machi 12, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. Itacheza ikiwa imetoka kucheza mechi ya marudiano dhidi ya Real Bamako kutoka nchini Mali. Baada ya mechi ya kwanza iliyochezwa jana, timu hizo zitacheza tena Machi 8, ikiwa ni za Kombe la Shirikisho barani Afrika, lakini siku nne baadaye itacheza mechi hiyo dhidi ya Geita Gold.

Inaweza kuwa mechi ngumu, au rahisi kwa Yanga kwa sababu kadhaa. Ngumu kwa sababu itakuwa inacheza siku chache baada ya kucheza mechi kubwa zenye matumizi makubwa ya nguvu na akili na huenda ikawachosha baadhi ya wachezaji wake muhimu.

Urahisi inakuja kwa sababu Yanga wachezaji wake wanaokaa benchi, angalau wana viwango vya kupambana na kushinda mechi hasa za Ligi Kuu. Pia Geita Gold ambayo inashika nafasi ya tano, haipo kwenye msitari mwekundu wa timu zenye hatari ya kushuka daraja na kusema kuwa huenda wachezaji wao watapambana kufa kupona.

**2. Yanga vs Kagera Sugar**

Faida nyingine ya Yanga ni kwamba mechi hii pia wanachezea kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa. Ni uwanja ambao timu zinazoitwa au kujiita za mikoani zinapata tabu sana zinapocheza na Simba na Yanga.

Aprili 7, mwaka huu, Yanga inakwenda kucheza dhidi ya Kagera Sugar kwenye uwanja huo. Kama mechi ya kwanza.

Itakuwa ni siku tano, baada ya kucheza mechi dhidi ya TP Mazembe mjini Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na hiyo itakuwa ni mechi ya mwisho ya Kombe la Shirikisho, Kundi D.

Ikiwa itafanikiwa kusonga mbele hatua ya robo fainali, itaongeza morali kwa viongozi, wachezaji na mashabiki wa timu hiyo kushinda mechi hiyo, bila kujali uchovu wa safari.

Lakini mechi inaweza kuwa ngumu kwa Yanga kama itashindwa kufuzu, kwani kisaikolojia wachezaji wa timu hiyo hawatokuwa vizuri.

**3. Simba vs Yanga**

Mechi ya watani wa jadi 'dabi' itapigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Aprili 16, mwaka huu. Ni mechi inayosubiriwa na mashabiki wengi wa soka kwani wanaona huenda ikaamua hatima ya timu zote mbili kwenye kutwaa au kuukosa ubingwa.

Wachambuzi wa masuala ya soka wanasema huenda mechi hii ndiyo ikawa ngumu kwa Yanga kuliko zingine na kama ni kupoteza, basi inawezakana ikawa ni hii.

Hata hivyo, kama Yanga ikishinda, basi hakuna wa kuizuia tena kwani itakuwa imebakisha mechi nne za kumalizia na endapo itashinda mechi zote tatu ikiwamo hiyo, itakuwa imebakisha ushindi kwenye mechi mbili tu kutwaa ufalme.

**4. Yanga vs Singida Big Stars**

Yanga itacheza dhidi ya Singida Big Stars kwenye Uwanja wa Liti, Singida mechi ambayo mpaka sasa bado haijapangiwa tarehe.

Ni kwa sababu ya michuano ya Kombe la Shirikisho inayoendelea. Hata hivyo, wachambuzi na wadadisi wa masuala ya soka wanasema kutokana na ukaribu wa timu hizo mbili, huenda ikawa mechi nyepesi sana kwao, hasa nyakati hizi ambazo inahitaji kila pointi ili kutimiza azma ya kutwaa ubingwa.

Wengine wanadai mechi itakuwa ngumu kama Singida Big Stars itakuwa inasaka pointi za kumaliza nafasi ya tatu ambayo moja kwa moja itakuwa inapata nafasi ya kucheza mechi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika msimu ujao.

**5. Yanga vs Dodoma Jiji**

Ni mechi nyingine ya Yanga ambayo inatajwa ni rahisi kama kumsukuma mlevi kwenye utelezi. Dodoma Jiji haijawahi kuwa mbishi kwa Yanga tangu ipande Ligi Kuu. Tena kwa bahati nzuri itachezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kwenye tarehe ambayo nayo itapangwa baadaye.

Inawezekana kabisa hii ikawa ndiyo moja ya mechi ambayo Yanga inakwenda kutwaa ubingwa Tanzania Bara.

Hata hivyo, ugumu unaweza kuja pale ambapo Dodoma Jiji nayo itakuwa inalazimika kusaka pointi za kuiwezesha kubaki Ligi Kuu kwani ipo kwenye hali mbaya. Kwa sasa inashika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 24.

**JE, WAJUA?**



WAKATI Newcastle na Manchester United zikicheza mechi ya Fainali ya Carabao Cup jana, hiyo ni mara ya kwanza kwa kikosi hicho cha Eddie Howe (Newcastle), kucheza fainali ya michuano ya ndani tangu 1999 ilipofungwa na 'Mashetani Wekundu' hao kwenye Fainali ya FA Cup.





## RC aagiza kutengwa maeneo ya uwekezaji kuvutia wageni

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amewataka wajumbe wa Baraza la Biashara la Mkoa ngazi ya wilaya kutenga maeneo ya uwekezaji ambayo yatavutia wageni kuwekeza katika halmashauri zao.

Senyamule aliyasema hayo jijini hapo alipokuwa akizindua baraza la biashara Mkoa huo lenye mpango mkakati wa kuifanya Dodoma kuwa kitivo cha biashara na uwekezaji nchini.

Alisema serikali imeendelea kuleta wawekezaji kutoka nje na wanaingia kwa wingi nchini hivyo lazima mkoa na halmashauri zake zitenge maeneo ambayo yatakuwa rafiki kwa wawekezaji pindi watakapokuja kuwekeza.

"Mkoa wa Dodoma tunataka tuwe na mchango mkubwa kwenye biashara hivyo ni matarajio yangu Baraza la Mkoa litakua bora na lenye utashi wa kipekee kwenye makao makuu ya nchi, hivyo nawaomba wajumbe wa baraza hilo ngazi ya wilaya kwenda kufanya vikao vya mabaraza pamoja na wale wa halmashauri," alisema na kuongeza:

"Wakurugenzi nao wakafanye hivyo, pia muende mkatenge maeneo ya uwekezaji ambayo yatavutia wageni watakapohitaji kwenda kuwekeza kwenye halmashauri zenu".

Kwa upande wake, Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatuma Mganga, alisema kuwa lengo la baraza hilo ni kuifanya Dodoma kuwa kitovu cha biashara nchini.

Alisema: "Malengo madogo yakiwa ni kuwa na mpango mkakati wa kufanya kazi ndani ya miaka mitatu, kutangaza shughuli za biashara na fursa za uwekezaji kupitia vyombo vya biashara, kuongeza idadi ya uwekezaji unaofanyika Dodoma, maeneo ya uwekezaji yaliyotwaliwa yapimwe ili yaboreshwe, mabaraza ya wilaya yaboreshwe pamoja na kuongeza wafanyabiashara."

# Halmashauri 34, mitaa 559 kupimwa, kupewa hati

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MENEJA wa Urasimishaji Ardhi Mijini kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Leon's Mwenda, amesema kuwa mradi wa kurasimishaji maeneo umejiwekea malengo ya kuzifikia halmashauri 34 nchini kupima na kutoa hati kwa mitaa 559.

Aliyasema hayo kwenye mkutano wa wananchi wa Kata ya Mbambala jijini hapo, alipokuwa akitoa elimu ya kuboresha miliki ya ardhi nchini.

Mwenda alisema hadi sasa kuna mitaa 1,436 ambayo hazijawahi kutambuliwa kupangwa, kupimwa na kumilikishwa, hivyo mradi huo utaenda kuifikia mitaa 559.

Alisema urasimishaji ulipanga kufikia mikoa 10 kwa kipindi cha mwaka 2013 hadi 2023 na mitaa 1961 ndio ambao imefikiwa kwa kupangwa na kupimwa makazi ambayo yameendelezwa bila kupangwa.

Meneja huyo alisema kuwa kutokana na mpango huo wa mradi wananchi wanatakiwa kujipanga katika kushirikiana na serikali kuhakikisha maeneo hayo yanapangwa kwa kuwa urasimishaji kwa wananchi utakuwa na faida kubwa ikiwa na pamoja kupata miundombinu ya barabara.

Awali akizungumza kwenye mkutano huo, Diwani wa Kata ya Mbambala, Paskadhia Mayala, aliwatoa hofu juu ya mradi huo kwa kuwataka washirikiane na serikali ili kukamilika kwa wakati. Alisema mradi huo hautawanyang'anya maeneo yao bali utakuwa na malengo ya uboreshaji miliki ya ardhi yenye malengo ya kuwawezesha kupata hati miliki zao za kwenye maeneo ambayo yameendelezwa bila kupangwa.

Aidha, alisema upimaji huo pia utaondoa migogoro iliyopo katika upatikanaji wa hati miliki na malalamiko ya viwanja nyumba na mashamba ukizingatia kuwa ni maelekezo kutoka serikalini.




Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dk. Alphonce Chandika, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma mwishoni mwa wiki akielezea majukumu na mafanikio ya hospitali hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Taasisi za dini zatakiwa kukemea vitendo vya ukatili

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

TAASISI za dini zimetakiwa kutumia nafasi zao kuisaidia serikali kukemea vitendo vya kikatili vilivyokithiri wanavyofanyiwa watoto, wanawake na watu wenye ulemavu.

Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Maendeleo ya Utamaduni, Dk. Julieth Kabyemela, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na viongozi wa dini wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG) Dodoma Kati wakati wa mkutano mkuu wa jimbo uliofanyika jijini hapo.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na taasisi hizo katika kutoa elimu na kukemea dhidi ya vitendo vya kikatili vinavyofanyika kwenye jamii na kuwataka viongozi hao kukemea na kutofumbia macho.

"Serikali bado inazitegemea taasisi za kidini katika kusaidia suala zima la utoaji na ukemeaji wa vitendo hivyo vya ukatili ambavyo vimesababishwa na kutoweka kwa mmonyoko wa maadili," alisema.

Alisema kwa kutumia nafasi zao wanafikia elimu kwa wana jamii na kuondokana na tabia hiyo ya vitendo vya kikatili vinavyogharimu maisha ya watu wasio na hatia.

"Serikali kwa upande wake bado inazitengemea taasisi za kidini, katika kutoa elimu na kukemea vitendo hivi vya kikatili vinavyofanywa na watu ambao hawana hofu na Mungu na kuhatarisha maisha ya wanadamu ambao wahawana makosa, wakiwamo watoto, wanawake na watu wenye ulemavu," alisema.

Naye Askofu wa Jimbo la Dodoma Kanisa hilo, Steven Mahinyila, alisema wanaunga mkono serikali katika kupambana na vitendo hivyo vya kikatili na kanisa litahakikisha linapeleka elimu kwenye shule za msingi na sekondari, ili kuwajengea uwezo imara wa kimaadili.

"Kwenye kongamano hili la wachungaji wa Jimbo la Dodoma kwa pamoja tumepitisha kuisaidia serikali katika mapambano haya ya kukemea kutoa elimu ili watu wanaojihusisha na vitendo hivyo wamgeukie Mungu na wawe watu wema," alisema.

Aidha katika mkutano huo kanisa hilo limepitisha utekelezaji wa mpango mkakati pia wakufungua makanisa na kuwasomesha wachungaji wao zaidi ya 70 na kuhubiri neno la Mungu kwenye maeneo mbalimbali.

lengo la mpango huo ni kuhakikisha watu wanakuwa na hofu ya Mungu na Tanzania iendelee kuwa na amani na utulivu huku wakifanya kazi zao kwa uhuru na kujipatia maendeleo ya kiuchumi na kiroho.

Aliwataka wachungaji hao kuiombea serikali na viongozi ili kuwasaidia kupambana na maovu ambayo yamekuwa yakirudisha nyuma maendeleo ya uchumi.





# TAZARA yaimarika kiuchumi, miundombinu yaboreshwa

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

SHIRIKA la Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), limeanza kuimarika kiuchumi baada ya serikali kuboresha miundombinu yake pamoja na kuruhusu sekta binafsi kuwekeza kwenye usafirishaji wa mizigo kupitia reli hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa TAZARA, Fuad Abdallah, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete katika Stesheni ya Mbeya kwa ajili ya kuangalia utekelezaji wa maagizo ya serikali.

Abdallah alisema mwaka 2015 serikali iliamua kuanza kulipa mishahara ya watumishi wa shirika hilo baada ya kushindwa kujiendesha jambo ambalo lilileta ahuweni kwenye uendeshaji.

Vilevile alisema mwaka 2017 serikali ilitoa Sh. bilioni 10 kwa ajili ya kufufua injini saba za treni zilizokuwa zimeharibika pamoja na kununua mitambo ya kuzalishia kokoto katika Mgodi wa Kongoro-Mswiswi ambako pia kuna kiwanda cha kuzalisha mataluma.

Alisema kabla ya mwaka 2015 shirika hilo lilikuwa lina uwezo mdogo wa kusafirisha mzigo lakini baada ya serikali kuingiza fedha zake, uwezo huo umeongezeka.

Alisema reli hiyo ina uwezo wa kusafirisha mzigo wenye uzito wa tani 5,000,000 kwa mwaka lakini mwaka 2014 shirika hilo lilisafirisha tani 80,000 pekee hali iliyoishtua serikali na kuanza kuchukua hatua za kulinusuru.

"Baada ya serikali kuingiza fedha zake kwa ajili ya kuboresha miundombinu, uwezo wetu umeongezeka na tuna uwezo wa kusafirisha zaidi ya tani 200,000 kwa mwaka jambo ambalo tunaona ni maendeleo makubwa," alisema Abdallah.

Alisema kwa sasa shirika hilo limeingia makubaliano na kampuni tatu ambazo zimewekeza kwenye usafirishaji wa mizigo kwenye reli hiyo ambayo kati yake mawili yameanza kufanya kazi na lingine lipo kwenye hatua za mwisho.

Alizitaja kampuni hizo kuwa ni Karabash LTD ya nchini Zambia na Africa Inland Container Depot LTD ya Tanzania ambayo yameshaanza kufanya kazi na BRAVO ya Tanzania ambayo bado haijaanza kufanya kazi.

Mwenyekiti wa uongozi wa shirika hilo katika Wilaya ya Tazara Mbeya, Betwel Kamugisha, alisema Stesheni ya Mbeya ni miongoni mwa stesheni ambazo zipo kwenye mpango wa ukarabati ili kuimarisha shughuli za shirika.

Alisema kwa sasa wameshapaka rangi kwenye majengo mbalimbali ya stesheni hiyo pamoja na kutengeneza viti kwa ajili ya abiria wanaosubiri gari moshi kukaa.

Alisema abiria ambao wanashuka katika stesheni hiyo wanakuwa zaidi ya 200 na wanaohitaji kukaa wanakuwa siyo chini ya 150 na wanahitaji viti zaidi ya 60 vyenye uwezo wa kukaliwa na watu watano kila kimoja lakini kwa sasa vipo 60.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwakibete, alilipongeza shirika hilo kwa kuanzisha utaratibu wa kuingia ubia na sekta binafsi kwenye matumizi ya miundombinu ya reli hiyo.

Alisema utaratibu huo ni mzuri na unatumika duniani kote na hivyo serikali inakusudia kuutumia kwenye reli zake zote ili kuongeza ufanisi kwenye usafirishaji.

Aliagiza uongozi wa shirika hilo kuingiza kwenye bajeti ya mwaka wa fedha ujao bajeti ya ununuzi wa viti kwa ajili ya kukalia abiria kwenye stesheni mbalimbali na kwamba wasipofanya hivyo serikali itapunguza matumizi ya kawaida na kuingiza kwenye ununuzi wa viti.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete (katikati), akitoa maelekezo kwa Mkurugenzi Mkuu wa Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), Fuad Abdallah (kushoto), kuhusu uboreshaji wa miundombinu katika stesheni ya Mbeya mwishoni mwa wiki alipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa maagizo ambapo aliagiza suala la ununuzi wa viti vya kukalia abiria wanaosubiri gari moshi liingizwe kwenye bajeti ijayo, (kulia) ni Mkuu wa Stesheni, Allen Masube. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Ujenzi wa Barabara Kiwanja -Ifumbo wamkosha mbunge

**Na Nebart Msokwa, CHUNYA**

MBUNGE wa Lupa wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, Masache Kasaka, ameridhishwa na ujenzi wa barabara ya Kiwanja – Ifumbo (kilomita 10) inayojengwa kwa kiwango cha changarawe akieleza kuwa itasaidia kuboresha mawasiliano.

Mwishoni mwa wiki Kasaka alifanya ziara ya kukagua barabara hiyo kwa lengo la kuangalia utekelezaji wake pamoja na kuzungumza na wananchi wa Kata ya Ifumbo ambao ndio wanufaika wa kwanza wa barabara hiyo.

Alisema barabara hiyo awali ilikuwa na hali mbaya na ilikuwa haiwezi kupitika kwa kutumia gari kutokana na kuwa na makorongo mengi hali iliyokuwa inawalazimu wananchi wa eneo hilo kutumia gharama kubwa kwenye usafiri.

Alisema usafiri ulikokuwa wa uhakika kutumika kwenye eneo hilo ilikuwa ni pikipiki na watembea kwa miguu lakini kwa wenye magari walikuwa wanashindwa kufika.

"Sasa naona imekuwa na hali nzuri na nina uhakika magari ya aina yoyote sasa yanaweza yakafika kwenye eneo hili, kwa hiyo niwaombe wananchi wa Ifumbo muitunze miundombinu hii," alisema Masache.

Aliwapongeza watendaji wa Wakala wa Barabara za Vijijini (TARURA) wilayani humo kwa kusimamia vizuri ujenzi wa barabara hiyo na kuifanya kuwa na uwezo wa kupitika mwaka mzima.

Alisema wilaya hiyo ina shida ya barabara zake nyingi kutopitika baadhi ya misimu hasa msimu wa mvua na hivyo akawataka kuendelea kuzifanyia maboresho barabara hizo mara kwa mara ili ziendelee kuwa na hali nzuri.

# H'shauri, wadau wazalisha miche ya kisasa ya kakao

**Na Nebart Msokwa, KYELA**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kyela kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa kakao imeanza kuboresha kilimo hicho kwa kuzalisha miche ya kisasa na kuigawa kwa wakulima ili kuongeza tija kwenye uzalishaji.

Halmashauri hiyo kwa kushirikiana na Chama Kikuu cha Wakulima wa Kakao wilayani humo (KYECU), wamezalisha zaidi ya miche 34,700 ya kakao ambayo imeanza kusambazwa kwa wakulima.

Akizindua ugawaji wa miche hiyo kwa wakulima juzi, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwataka wakulima kuitumia miche hiyo na kuondokana na ile ya zamani ambayo tija yake kwa sasa imekuwa ndogo.

Alisema wakulima wamekuwa wakitumia miche hiyo ya zamani kwa muda mrefu hali ambayo imeanza kushusha uzalishaji kutokana na baadhi yake kufa na mingine kuanza kushambuliwa na magonjwa.

Alisema kitendo cha halmashauri hiyo kuzalisha miche hiyo na kuigawa bure kwa wakulima kinaashiria kuanza kufufuka kwa zao hilo ambalo miaka ya karibuni lilianza kushuka.

Aliwataka wakulima kuwa huru kuhifadhi mazao yao kwenye ghala lolote ambalo wanataka badala ya kulazimishwa kuhifadhi kwenye baadhi ya maghala na vyama vyao vya msingi.

Pia aliwataka wakulima wanaogawiwa miche hiyo kuitunza vizuri ili ikuwe na iwasaidie kuongeza kipato huku akisisitiza kuwa wasipoitunza watasababisha halmashauri kukata tamaa.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Josephine Manase, alisema waliamua kuanza kuzalisha miche kutokana na zao hilo kuwa ndilo zao kuu la biashara kwa wilaya hiyo na ni miongoni mwa vyanzo vya mapato ya halmashauri.

Alisema miche hiyo ina uwezo wa kuanza kuzaa mapema hata kipato chake ni kikubwa kuliko ile ya asili ambayo wakulima wamekuwa wakiitumia kwa zaidi ya miaka 20.

Alisema ili kuhakikisha wakulima wanaipanda miche hiyo vizuri, serikali imewaelekeza maofisa ugani kuhakikisha wanawasaidia wakulima hao mbinu za kitaalamu za kuipanda na kuihudumia.

Baadhi ya wakulima waliishukuru serikali kwa kuamua kuwasaidia kuzalisha miche hiyo kwa maelezo kuwa itawasaidia kuondokana na kilimo cha mazoea.

Mmoja wa wakulima hao, Francis Mwambungu, alisema miche ya zamani kwa sasa hivi imeanza kuwaongezea gharama za uzalishaji kutokana na kuanza kuvamiwa na wadudu pamoja na magonjwa.



## China yakubali kuwekeza kwenye uchumi wa buluu

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar kimesema kuwa Serikali ya China imekubali kuwekeza katika miradi mbalimbali inayobeba dhana ya uchumi wa buluu.

Naib Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Mohammed Said Mohammed 'Dimwa', alibainisha hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukamilisha ziara ya ujumbe wa Chama cha Kikomunisti cha Chini visiwani Zanzibar.

Alisema Serikali ya China imekubali kuwekeza katika bahari hasa katika mazao ya baharini ikiwa mo mwani, uvuvi na ufugaji wa kaa.

Alisema mbali na kuwekeza katika miradi hiyo pia wamekubaliana kuwekeza katika miradi ya CCM Zanzibar kwa kujenga nyumba za watumishi zitakazouzwa kwa gharama nafuu ili viongozi, watumishi na watendaji wa CCM wapate makaazi bora ya kuishi.

"Ziara hii imekuwa na mafanikio makubwa kwani tumejadili mambo mengi ya msingi yanayolenga kutatua kero za wananchi na wanachama wa CCM kwa ujumla," alisema Dk.Dimwa.

Dk .Dimwa alisema CCM inawakaribisha wawekezaji wa ndani ili waweze kuwekeza huku ikifungua milango kwa wawekezaji wa kimataifa.

Katibu wa Kamati Maalum ya NEC, Idara ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (SUKI), Khadija Ali Salum, alisema lengo la ziara hiyo ni kuimarisha uhusiano katika nyanja za utamaduni, siasa, diplomasia, uchumi, jamii, michezo na burudani na uwekezaji.

Alieleza kuwa kwa miaka mingi Chama Cha Kikomunist cha China (CPC) na CCM vimekuwa ni vyama vyenye urafiki na undugu wa kihistoria katika masuala ya kuimarisha Ilani za uchaguzi za vyama hivyo.

Alisema ujumbe wa CPC ulipowasili Zanzibar wamevutiwa na mazingira ya Zanzibar na wakaweka wazi nia yao ya kuja kuwekeza katika sekta ya bahari katika masuala ya usafiri, uvuvi na kilimo cha baharini cha mwani.

Mkuu wa Idara ya SUKI, Khadija, alisema kuwa CCM inaendelea kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia na vyama mbalimbali duniani ili kwenda sambamba na siasa ya kisayansi inayojikita katika masuala muhimu ya kuondosha changamoto na kero za wananchi kwa wakati.

# Idadi ya watalii walioingia Z'bar Januari yaongezeka

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KATIKA kipindi cha Januari mwaka huu raia wa kigeni 68,813 waliingia Zanzibar, idadi ambayo iliongezeka kwa asilimia 3.1 kulinganisha na wageni 66,720 waliingia Desemba mwaka jana.

Mkuu wa Divisheni ya Utoaji Huduma Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Bakari Khamis Kondo, alibainisha hayo jana wakati akiwasilisha takwimu za uingiaji wageni huko Mazizini.

Alisema idadi hiyo ya wageni imeongezeka kwa asilimia 62.1 ukilinganisha na wageni 42,443 waliongia nchini kwa kipindi cha Januari 2022, hali inayoonesha kuendelea kuimarika kwa sekta hiyo baada ya janga la ugonjwa wa virusi vya corona.

Alisema kati ya idadi hiyo wageni wengi walitoka Itali ambao waliingia watalii 10,338 sawa na asilimia 15.0 ya wageni wote ikifuatiwa na Ufaransa iliyokuwa na wageni 1,658 (asilimia 12.6).

Mataifa mengine ni Poland (6,102), Ujerumani (4,364) na nchi za Scandnavia wageni 3,588 sawa na asilimia 5.2.

Alisema asilimia 52.3 ya wageni walikuwa wanawake na wanaume walikuwa asilimia 47.7 ambapo asilimia 89.7 ya wageni hao walikuja nchini kwa ajili ya mapumziko.

Mchumi Mwandamizi Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Dk. Ulrick Mumburi, alisema, kuongezeka kwa watalii kutaistawisha zaidi Zanzibar ambayo utalii umekuwa ndiyo tegemeo la kiuchumi.

"Utalii ni mapato ya serikali, ndiyo za fedha za kigeni, ni ajira, unachangia kwa kiasi kikubwa pato la taifa." Alisema.

Hivyo alisema kuongezeka kwa idadi ya wageni ni kuifungua nchi kiuchumi kulingana na sera na mikakati ya nchi katika kufikia malengo iliyojiwekea.

Alisema kwa Januari makusanyo yote ya kodi yalifikia shilingi bilioni 89.6 ambapo ni ufanisi wa ukusanyaji imefikia asilimia 92 ya malengo na hiyo inaakisiwa na idadi ya watalii kuongezeka.

Naye Ofisa Tafiti za Utalii Kamisheni ya Utalii, Maabadi Jaffar Mwadini, alisema afueni ya janga la corona imechangia kuongezeka utalii duniani ambapo kulingana na Shirika la Utalii Duniani, zaidi ya watalii milioni 900 walisafiri katika nchini mbalimbali.

Alisema hali hiyo inadhihirisha afueni ya kurejea kwa utalii ilikuwa kwenye kiwango bora kwa mwaka 2022 baada ya janga la corona 2019-2021.

Alisema inakadiriwa kwa mwaka 2023 kiwango cha ukuaji wa utalii kikafikia asilimia 50 mpaka 70 huku Zanzibar ikinufaika na ukuaji huo wa utalii duniani.



Naibu Katibu wa Idara ya Itikadi na Uenezi wa CCM Zanzibar, Khamis Mbeto, akiwa katika hafla ya uzinduzi wa ahadi ya Chama cha ACT-Wazalendo iliyofanyika Mtoni Zanzibar mwishoni mwa wiki. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Sheria ya watu wenye ulemavu kuleta fursa na maendeleo

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MWAKILISHI wa Viti Maalum, Mwantatu Mbaraka Khamis, amesema Sheria ya Watu Wenye Ulemavu iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi hivi karibuni imefunguwa milango kwa watu wenye ulemavu.

Hivyo aliwataka wanawake wenye ulemavu kuitumia haki ya kikatiba kuwania nafasi hizo ili kupaza sauti na kuleta mabadiliko makubwa katika jamii kulingana na mahitaji yao.

Aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya wiki moja kwa wanawake wa wanachama wa Jumuiya ya Wanawake wa Wenye Ulemavu (JUWAUZA) huko Jambiani Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema bado wanawake wenye ulemavu hawana mwamko wa kuwania nafasi za uongozi na matokeo yake nafasi hizo zikichukuliwa na watu wingine.

Alisema mabadiliko yaliyofanywa na Baraza la Wawakilishi kwa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu sasa inatoa nafasi zaidi kwa makundi yote kushiriki katika uchaguzi ambapo wamejipanga kuhakikisha sheria hiyo wanakwenda kuisimamia.

Alitoa mfano wake akisema katika mwaka 2005 aligombea nafasi ya uwakilishi kupitia nafasi za watu wenye ulemavu katika Mkoa wa Kusini na alikosa lakini hakukata tamaa na kushiriki tena katika kinyang'anyiro hicho katika mwaka 2010 na kushinda.

Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee Watoto, Abeda Abeid Rashid, alisema Serikali ya Zanzibar imetoa fursa nyingi za uongozi kwa wanawake wenye ulemavu ikiwamo katika vyombo vya kutunga sheria kwa kuteua wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watatu.

Aidha, alisema Rais wa Zanzibar Dk.Hussein Ali Mwinyi, amewaunganisha watu wenye ulemavu kwa kuwasilishwa kwa sheria mpya ya watu wenye ulemavu ambayo imebainisha fursa nyingi zinazoweza kutumiwa ikiwamo haki na fursa za kushiriki katika uongozi wa kisiasa.

Mfuatiliaji wa miradi katika Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu, Suleiman Mujuni, alisema mafunzo hayo yamelenga katika kuwajengea uwezo wanawake wenye ulemavu kushiriki katika harakati za kisiasa za ushindani ikiwamo katika majimbo ya uchaguzi.

# TANMET yajivunia kuchochea maendeleo ya elimu nchini

Na Maulid Mmbaga

MTANDAO wa Elimu Tanzania (TENMET) umesema umefanikiwa kuchochea maendeleo ya elimu nchini tangu ulipoanza kuratibu mradi wa ufuatiliaji na kufanya tathmini ya kazi zinazofanyika kwenye jamii kupitia fedha zilizotolewa.

Programu hiyo inayosimamiwa na TENMET ilianza utekelezaji wa majukumu yake Septemba 2022 na inatarajiwa kukamilisha Machi mwaka huu.

Jana ilikutana na taasisi 10 inazoshirikiana nazo katika utekelezaji wa mradi huo unaofanyika kwenye mikoa 10 ambayo ni Dodoma, Rukwa, Katavi, Pwani, Njombe, Iringa, Morogoro, Mtwara, Tanga na Lindi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, Msimamizi wa Programu hiyo wa TENMET, Matha Makala, alisema matokeo waliyoyapata ndani ya miezi sita katika utekelezaji wa mradi huo ni kuanzishwa kwa kamati za ufuatiliaji na tathmini ya rasilimali za umma kwenye sekta ya elimu katika maeneo ambayo hayakuwa nazo.

Pia alisema mradi huo umechochea ujenzi wa miundombinu ambayo haikuwa imekamilika ukiwamo wa vyoo na madarasa na kwamba kamati ziliamsha ari na kuonyesha umuhimu wa wananchi kwenye kufuatilia rasilimali za umma.

"Kamati ziliongezea uelewa jamii juu ya umuhimu wa wananchi katika kuchangia kwenye sekta ya elimu kwa sababu kazi ya kuchangia kuboresha sekta hii sio ya serikali peke yake, badala yake inaihusu pia wananchi na taasisi binafsi (NGO) katika kuhakikisha hizi kazi zinafanyika.

"Tumeona wananchi kwenye maeneo ya utekelezaji wa mradi wakishiriki kukamilisha majengo na vyoo ambavyo vilikuwa havijakamilika, kufyatua matofali na kutoa maeneo ambayo walikuwa wameyaweka kama mashamba kwa ajili ya kufanya ujenzi wa madarasa ili kuhakikisha wanachangia katika kutatua tatizo la madarasa," alisema Matha.

Alibainisha kuwa anaona jamii inaamka katika kufuata nyayo ambazo ilitakiwa kufanya kwa kushirikiana na serikali kuhakikisha upatikanaji wa madarasa na kutumia rasilimali zilizoko kwenye maeneo yao ili watoto wanufaike nazo.

Alisisitiza umuhimu wa ushirikishwaji wa wananchi katika masuala ya kijamii, akieleza kuwa watasaidia kuendeleza miradi inayoanzishwa kwenye maeneo husika.

Samson Mnyawami wa Taasisi ya MMADEA, inayotekeleza mradi huo mkoani Morogoro, alisema katika utekelezaji wa programu hiyo walibaini kuwapo upungufu wa vifaa vya kufundishia ikiwamo vitabu kwenye shule na kutokuwa na uwiano sahihi wa walimu na wanafunzi kwa darasa moja, kukiwa na zaidi ya wanafunzi 80 kwa darasa.

Alisema walibaini pia kuwa miundominu kwa watoto walemavu ni tatizo, akieleza kuwa changamoto zingine walizozibaini ni upungufu wa madarasa, nyumba za walimu, uhusiano hafifu wa taasisi za elimu na zingine na unyanyasaji wa kijinsia.

Mratibu wa Taasisi ya Green Leaf, Arnold Limbu, watekelezaji wa mradi huo Mkoa wa Katavi, alisema wamefanikiwa kuhamasisha ushiriki na ushirikishwaji wa jamii katika ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma katika miradi ya maendeleo kwenye shule za msingi za Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

Mratibu huyo alibainisha kuwa katika utekelezaji wa majukumu yao walikutana na changamoto ya ushirikiano mdogo kutoka kwa viongozi wa eneo husika, licha ya kuwa na nia njema ya kuboresha mazingira ya elimu nchini.

Shaibu Lipwata wa Taasisi ya Tarukudefu inayotekeleza mradi huo mkoani Pwani, alisema moja ya majukumu waliyoyafanya ni kuzijengea uwezo kamati zilizoundwa ili zifuatilie kwa ufanisi maendeleo ya elimu kwenye eneo husika.

Alieleza kuwa changamoto walizozipata wakati wa utekelezaji wa mradi ni kuwapo siasa katika mradi na jamii ilikuwa inashindwa kuamini mradi wakidhani kwamba waratibu ni washiriki wa siasa kutoka chama fulani.



Wanachama wa CCM Wilaya ya Liwale mkoani Lindi wakishiriki matembezi katika maadhimisho ya Wiki ya Chipukizi wa chama hicho mjini Liwale jana. **PICHA: MPIGAPICHA**

# Benki yajitosa mkakati kukuza Utalii Zanzibar

Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR

BENKI ya Exim Tanzania imeahidi kuunga mkono jitihada za ukuzaji wa Sekta ya Utalii Zanzibar, ili kufikia lengo la kuongeza idadi ya watalii hadi 850,000 kila mwaka ifikapo 2025.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Jaffari Matundu, alitoa ahadi hiyo mbele ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, aliyetembelea banda la benki hiyo wakati wa mkutano wa wadau wa Utalii Zanzibar (Z -Summit) uliomalizika mwishoni mwa wiki visiwani hapo.

Akielezea huduma zinazotolewa na benki hiyo mahusus kwa wadau wa utalii visiwani humo, Matundu alisisitiza dhamira ya Exim katika kuboresha sekta hiyo, akibainisha kuwa wamejipanga kukuza maendeleo jumuishi na kuwasaidia wajasiriamali wa utalii wa ndani, wakiwamo wanawake na vijana kutumia mifumo ya kidijitali kukuza biashara zao.

"Benki ya Exim kupitia mipango mbalimbali, imetoa mwelekeo mpya katika maendeleo ya utalii. Kwa kuwasiliana na timu yetu iliyojizatiti kupitia dawati maalum la kuhudumia wadau wa utalii Zanzibar, wadau wa utalii wameweza kunufaika kwa kupata huduma za kifedha zinazoendana na mahitaji yao kwa wakati sahihi na hivyo kuongeza tija katika uendeshaji wa shughuli zao," alisema.

Benki ya Exim Tanzania ilikuwa mdhamini mkuu wa mkutano huo wa kwanza wa kimataifa uliofanyika Zanzibar kupitia uratibu wa Jumuiya ya Wawekezaji wa Utalii Zanzibar (ZATI) kwa kushirikiana na Kilifair, ukihudhuriwa na wajumbe zaidi ya 300 kutoka Sekta ya Utalii wakiwamo viongozi waandamizi wa serikali pamoja na watoa huduma za watalii, wakujumuisha wamiliki wa hoteli.

Kwa mujibu wa Matundu, kwa kushirikiana na ZATI, mwaka mmoja uliopita, benki hiyo imefanikiwa kurahisisha utoaji wa huduma zake za kifedha kwa wanachama wote wa ZATI, ikiwamo mikopo ya kampuni na wafanyabiashara wadogo kulingana na mahitaji yao, pia kutoa huduma za kubadilishia fedha kwa bei shindani.

Nyingine ni pamoja na huduma za kipaumbele kwa wadau wa utalii kwenye matawi ya benki hiyo, kuwapo meneja uhusiano mahususi kwa ajili ya wadau wa utalii kwenye tawi hilo, huduma ya usafirishaji wa fedha, huduma za Bima na Mashine za Malipo (POS), ili kurahisisha malipo kwa watalii na hivyo kuondoa ulazima wa kubeba au kutembea na fedha.

"Ushirikiano huo ni mfano wa msaada wa muda mrefu na mkubwa ambao Benki ya Exim inatoa kwa sekta hii ya utalii Zanzibar," alisema.

Katika hotuba yake ya ufunguzi, Dk. Mwinyi, aliishukuru sekta binafsi na wadau wengine wa utalii kwa kushirikiana na serikali kutangaza visiwa hivyo.

Alisema utalii unachangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa Zanzibar, ukichangia karibu asilimia 30 ya pato la nchi, serikali yake ikidhamiria kukidhi mahitaji ya soko kwa kuhakikisha upatikanaji wa watalii 850,000 kwa mwaka ifikapo mwaka 2025.

# Shule shikizi mbioni kukamilika Chalinze

Na Julieth Mkireri, CHALINZE

WATOTO wanaoishi Kijiji cha Manda Mazingira, Kata ya Mkange, wako mbioni kuondokana na kikwazo cha kutembea umbali mrefu kupata elimu baada ya shule shikizi ya Kwamakuru kufikia hatua za mwisho za ujenzi.

Imebainishwa kuwa kwenye Kitongoji cha Kwamakuru, wapo watoto wengine waliokuwa wanakwama kwenda shuleni kutokana na umbali mrefu wa kuifikia shule, hivyo wengi kukatisha masomo.

Akizungumza juzi wakati Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Chalinze ilipotembelea shule hiyo kukagua matumizi ya fedha zilizotolewa na mfuko huo, Diwani wa Mkange, Mohamed Gelegeza, alisema wapo watoto wanaoshindwa kuanza masomo kutokana na umbali.

Gelegeza alimshukuru Mbunge Ridhiwani Kikwete na kamati ya matumizi ya fedha za mfuko huo kwa kuidhinisha fedha kutoka kwenye mfuko huo kwa ajili ya kujenga vyumba vya madarasa vya shule hiyo ambayo inatarajiwa kukamilika hivi karibuni ili isajiliwe.

Alisema kuwa kwenye Kata ya Kibindu, wananchi wanatarajia kuondokana na kikwazo cha kutembelea umbali wa kilomita 20 hadi 22 wakifuata huduma za afya baada ya kuanzisha ujenzi wa zahanati eneo la Kwakonje ambapo mfuko wa jimbo umetoa fedha kuchangia.

Diwani wa Kibindu, Ramadhani Mkufya alishukuru kwa fedha za uendelezaji wa ujezi huo ambao umeanzishwa na wananchi huku akiomba halmashauri isaidie kukamilisha mradi huo.

Kaimu Mwenyekiti wa Mfuko huo, Malota Kwaga, alisema fedha za mfuko huo zimekuwa zikichochea maendeleo ya wananchi kwa kujikita zaidi kutekeleza miradi iliyoanzishwa ambayo inakwenda kuondoa vikwazo vilivyoko.

Kwaga alisema miradi mingi inayotekelezwa na mfuko huo ni ile iliyoibuliwa na wananchi baada ya kuwa na kikwazo cha muda mrefu kwenye maeneo yao.

Kaimu Ofisa Mipango wa Halmashauri hiyo, Rugambwa Matui, alisema atafikisha maombi hayo serikalini ili itenge kutenga fedha za kukamilisha miradi iliyoanzishwa.

# AU yalaani maneno ya Rais Saied

**ADDIS ABABA, Ethiopia**

UMOJA wa Afrika (AU) umelaani matamshi ya Rais wa Tunisia, Kais Saied, kuhusu wahamiaji kutoka Kusini mwa Jangwa la Sahara na kuzitaka nchi wanachama wake kujiepusha na matamshi yoyote ya chuki ya asili ya kibaguzi ambayo yanaweza kuwadhuru watu.

Jumanne, Rais Saied alitetea hatua za dharura dhidi ya uhamiaji haramu wa raia wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, akisema kuwa uwepo wao nchini Tunisia ni chanzo cha vurugu, uhalifu na vitendo visivyokubalika, matamshi yaliyokashifiwa na mashirika yasiyo ya kiserikali.

Kwa mujibu wa takwimu rasmi zilizonukuliwa na Shirika la Haki za Kiuchumi na Kijamii la Tunisia (FTDES), taifa hilo lenye wakazi milioni 12, lina zaidi ya raia 21,000 kutoka nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, wengi wao wakiwa katika hali isiyo ya kuridhisha.

Wakati wa mkutano, pia Rais Saied alitoa matamshi makali kuhusu kuwasili kwa makundi ya wahamiaji haramu na alisisitiza haja ya kukomesha haraka kwa uhamiaji huo.

Katika taarifa iliyotolewa mwishoni mwa juma lililopita, Mwenyekiti wa Kamisheni ya AU, Moussa Faki Mahamat, alilaani vikali matamshi ya kushtua yaliyotolewa na mamlaka ya Tunisia dhidi ya Waafrika wenzao, ambayo yanakwenda kinyume na barua na moyo wa umoja huo na kanuni zao za msingi.

"Inazikumbushwa kwa nchi zote, hasa nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, kwamba lazima ziheshimu majukumu yao chini ya sheria ya kimataifa, yaani kuwatendea wahamiaji wote utu, popote wanapotoka, wajiepushe na matamshi ya chuki ya asili ya kibaguzi, uwezekano wa kuwadhuru watu, na kutoa kipaumbele kwa usalama wao na haki zao za kimsingi," alisema Mahamat.

Aliongeza kwa kusisitiza dhamira ya tume ya kuunga mkono mamlaka ya Tunisia katika kutatua masuala ya uhamiaji ili kufanya uhamiaji kuwa salama, wenye heshima na wa kawaida nchini humo.

Katika taarifa nyingine Ubalozi wa Mali nchini Tunisia ulisema unafuatilia kwa wasiwasi mkubwa hali ya raia wa Mali nchini humo.

Hata hivyo ubalozi huo ulitoa wito kwa raia wake kuwa macho na watulivu, huku ukiwaomba wale wanaotaka kujiandikisha kurudi nyumbani kwa hiari kufanya hivyo haraka iwezekanavyo.

***RFI***

## Spain yatangaza kesi ugonjwa wa Marburg

**MADRID, Spain**

TAIFA la Spain limeripoti kesi ya kwanza inayoshukiwa kuwa ya maambukizi ya ugonjwa wa Marburg kutoka kwa mgonjwa mwenye umri wa miaka 34 aliyerejea nchini humo hivi karibuni baada ya ziara nchini Equatorial Guinea.

Kwa mujibu wa maofisa wa afya wa nchini humo, mwanzoni mgonjwa huyo alikuwa amelazwa kwenye hospitali binafsi, lakini sasa amehamishiwa katika wodi maalum iliyotengwa kwenye Hospitali ya La Fe Valencia.

Pia kwa mujibu wa Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa cha (CDC), ugonjwa wa Maburg husababishwa na virusi ambavyo husababisha kuvuja damu miongoni mwa wanadamu na nyani na unaweza kusababisha vifo.

Maofisa wa Uhispania walisema kwamba zaidi ya watu 200 nchini Equatorial Guinea wamegundulika kuwa na maradhi ya Marburg katika siku za karibuni.

Mapema mwezi huu, kesi mbili za maambukizi ya ugonjwa huo yalipatikana nchini Cameroon karibu na mpaka wake na Equatorial Guinea.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linasema kwamba ugonjwa huo unaosababishwa na virusi unaweza kusababisha vifo kwa asilimia 88 ya wagonjwa, ukiwa kwenye kundi moja na ule wa virusi vya ebola.

***VOA***




Maofisa wa uchaguzi wakiendelea kuhesabu kura nchini Nigeria baada ya uchaguzi wa urais na wabunge uliofanyika juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Kura zaendelea kuhesabiwa, maswaibu lukuki yaripotiwa

**ABUJA, Nigeria**

SHUGHULI za kuhesabu kura zinaendelea katika uchaguzi wa urais nchini Nigeria, huku machafuko mbalimbali yakiripotiwa ikiwamo kushambuliwa kwa wasimamizi wa vituo, kuibwa kwa masanduku ya kura na wananchi kulazimishwa kumpigia kura mgombea fulani.

Idadi ya watu waliojitokeza kupiga kura juzi iliripotiwa kuwa juu, huku vijana wengi wa wapigakura wa mara ya kwanza wakifika kabla ya mapambazuko ili kutimiza haki yao ya kikatiba.

Inaelezwa kuwa upigaji kura wa Jumamosi ulitawaliwa na ucheleweshaji wa muda mrefu katika vituo vya kupigia kura, pamoja na ripoti zilizosambaa za unyakuzi wa masanduku ya kura na mashambulizi ya watu wenye silaha.

Pia baadhi ya vyama viliibua hofu juu ya madai ya ukiukwaji wa sheria, jambo ambalo linaweza kusababisha matokeo yenye utata.

Inabainishwa kuwa kumekuwa na changamoto kubwa kutoka kwa mgombea wa chama cha tatu katika kinyang'anyiro cha kumrithi Rais Muhammadu Buhari wa Chama cha Labour, ambaye anaungwa mkono na vijana wengi.

Makumi kwa maelfu ya vituo vya kupigia kura vinahesabu matokeo, ambayo yatakusanywa na kutumwa kwenye makao makuu ya uchaguzi katika mji mkuu wa Abuja, huku matokeo ya mwisho yakitarajiwa kutolewa kesho.

Mkuu wa Uchaguzi, Mahmood Yakubu, aliomba radhi kwa kucheleweshwa kwa upigaji kura, bila kutoa sababu za ucheleweshaji huo.

**MASANDUKU KUIBWA**

Hata hivyo inabainisha kuwa siku ya uchaguzi kwa kiasi kikubwa ilikuwa ya amani, licha ya uwapo wa taarifa za ghasia kutoka Mjini Lagos kwamba masanduku ya kura yaliibiwa.

Baadhi ya wapigakura walilalamikia kushambuliwa na kufukuzwa walipokuwa wamekusanyika kupiga kura.

Katika maeneo mengine, watu waliripotiwa kuombwa ama kumpigia kura mgombea fulani au kuondoka katika kituo cha kupigia kura.

Vile vile, msimamizi wa uchaguzi Yakubu, alisema watu waliokuwa na silaha pia walishambulia baadhi ya vitengo vya kupigia kura katika jimbo la kusini la Delta na jimbo la kaskazini la Katsina na kwamba mashine za kuthibitisha kadi za wapigakura zilibebwa na watu wasiojulikana.

Inaelezwa kuwa ya muda mchache kulipelekwa mashine zingine na usalama kuimarishwa ili kuruhusu upigaji kura kufanyika.

Ilibainishwa kuwa upigaji kura uliahirishwa hadi jana katika vituo 141 vya kupigia kura katika jimbo la Bayelsa kusini kwasababu ya kutatizwa kwa shughuli hiyo.

Katika jimbo la kaskazini mashariki la Borno, Yakubu alisema kwamba wanamgambo wa Kiislamu waliwafyatulia risasi maofisa wa uchaguzi kutoka kilele cha mlima eneo la Gwoza, na kuwajeruhi kadhaa.

***BBC***

# MABINGWA 'BETIKA MTOKO' DABI SIMBA, YANGA WAONGEZEKA

**Mwandishi Wetu**

ZIKIWA zimesalia siku 47 kabla ya mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga kupigwa Aprili 16, mwaka huu, washindi wa 'Betika Mtoko wa Kibingwa', wamezidi kuongezeka tayari kuushuhudia mtanange huo laivu.

Mashabiki 100 watakaoshinda kwenye Promosheni ya Betika Mtoko wa Kibingwa wataishuhudia dabi hiyo ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, bure kwa gharama za kampuni ya kubashiri matokeo ya Betika Tanzania.

Mpaka sasa, mikoa ya Kanda ya Ziwa inaongoza kwa kutoa washindi wengi kwenye promosheni hiyo, watano kati ya 14 waliopatikana kwa wiki mbili wanatokea mikoa hiyo.

Washindi hao ni Bahame Masangwa Balele (Simiyu), Stephano Skaut Charles na Joram Pius (Kagera), Paschal David John (Geita) na Jovin Joseph Rwakatare (Mwanza).

Wengine kutoka mikoa mingine ni Constantine Constantine Mbele (Ruvuma), Mariam Mohamed Ramadhan na William Athuman (Dar-es-Salaam), Joshua Charles Gasado (Morogoro), Salivius Lucas Frugence na John Nodi Nyato (Njombe), Richard Moris Mbewe (Rukwa), Elias Ezekiel Msongole (Mbeya) na Said Mohammed wa Moshi, Kilimanjaro.

Ofisa Habari wa Betika Tanzania, Juvelinaus Rugambwa, alisema promosheni hiyo inawapa fursa wateja wa Betika kushinda tiketi ya ndege kwenda Dar es Salaam kushuhudia dabi hiyo kwa gharama za Betika.

"Hamasa ni kubwa, tayari washindi 14 wamepatikana, katika awamu hii ya tano ya Mtoko wa Kibingwa yenye kauli mbiu 'Haina mbambamba' hata kama mkeka wako umechanika kwenye Jackpoti, bado una fursa ya kuingia kwenye promosheni hii, unachotakiwa ni kucheza mara tano kwa kuanzia Sh. 500 na kuendelea," alisema.

Alisema washindi wameanza kufanyiwa usajili huku kuanzia leo hadi Ijumaa kutakuwa na droo nyingine kupata washindi wa wiki hii, na kwamba unachotakiwa ni kuendelea kucheza na Betika na moja kwa moja utaingia kwenye Mtoko wa Kibingwa bila kujali kama mkeka wako umetiki au umechanika.

## KILI MARATHON...



Baadhi ya wafanyakazi wa Benki ya Biashara ya DCB, wakishiriki mbio za kilomita 21 za Kimataifa za Kilimanjaro Marathon mjini Moshi, Kilimanjaro jana. **MPIGAPICHA WETU**

# Kocha KMC alia marefa kuibeba Azam

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa KMC, Mrundi Thierry Hitimana, amelia na waamuzi waliochezesha mechi yao juzi dhidi ya Azam FC, wakiongozwa na refa wa kati Isihaka Mwalile, kwa kushindwa kuwapa penalti mbili za wazi ambazo walistahili.

Hitimana ambaye timu yake ilifungwa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Azam Complex, lililozamishwa kambani na Idd Nado, alisema waamuzi hawakuitendea haki timu yao kiasi hata baadhi ya wachezaji wa Azam walionekana kuwaonea huruma.

Hatukufeli kwenye mechi hii, tumecheza vizuri, kuna vitu vingine tunalalamika, lakini tunaonekana kama vile walalamishi, unajua ukiwa timu ndogo ni matatizo sana, hatukutendewa haki, kuna penalti mbili za wazi ilibidi tupewe, lakini ziliachwa tu, hata baadhi ya wachezaji wa Azam FC ambao ni mabeki waliosababisha, pambano lilipomalizika walinifuata kunipa pole, wakaniambia kocha pole sana zile zilikuwa penalti kabisa, wamewadhulumu tu.

"Basi tunakubali, nawapongeza wachezaji wangu, tulicheza mechi ngumu mbili kwa muda mfupi tena na timu zilizopo juu, tulicheza na Yanga, halafu hii na Azam, nadhani mechi zilizobaki tutapambana ili tusishuke kwenye msimamo wa ligi zaidi ya hapa tulipo," alisema Hitimana.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Azam, Aggrey Morris, alisema wameyapokea vema matokeo hayo, akiwapongeza wapinzani wao KMC kwa kucheza vizuri.

"Tumeyapokea vizuri, KMC wamecheza vizuri, ushindi kwetu ni furaha, mechi tunaimaliza haya wamepita tunaangalia mbele hizo zinazokuja," alisema nahodha huyo wa zamani wa timu hiyo. Kwa matokeo hayo, Azam inaendelea kushika nafasi ya tatu, ikifikisha pointi 47, ikiwa imebakia na mechi sita kumaliza msimu huu, huku KMC ikiwa kwenye nafasi ya 13, ikisalia na pointi zake zile zile 23.

## Mmarekani aja na Reggae Tanzania

**Na Frank Monyo**

MSANII wa Muziki wa Reggae kutoka New York, Marekani, Nat Sterling, anatarajia kutua nchini mwezi ujao kwa ajili ya ziara pamoja kutambulisha albumu yake mpya inayojulikana kwa jina la 'Side of the Time' kupitia maonyesho mbalimbali anayotarajia kuyafanya.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mratibu wa ziara ya msanii huyo, Dimateo Zion, alisema maandalizi ya msanii huyo wa Reggae kutoka New York, Marekani kuja Tanzania, yanaendelea vizuri na anatarajia kuwasili hivi karibuni.

Zion alisema lengo la ziara hiyo ni kutambulisha albamu yake kwa wadau wa nyimbo za reggae pamoja na kushirikiana na wasanii wengine hapa nchini katika kuhakikisha muziki wao huo unasonga mbele.

"Anatarajia kutambulisha nyimbo 12 kupitia maonyesho mbalimbali atakayofanya, tunawaomba Watanzania kutoa ushirikiano kwa msanii huyo wa kimataifa kutoka New York, Marekani," alisema Zion na kuongeza:

## KMKM yapunguzwa kasi ubingwa Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya KMKM imepunguzwa kasi ya kuukaribia Ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya juzi kupokea kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Maafande wa Uhamiaji FC.

Bao pekee lililoizamisha 'manuari' ya KMKM lilipachikwa nyavuni na Abdul Hafidh katika dakika ya 88.

Kwa KMKM kupoteza mchezo huo kunatoa mwanya kwa mpinzani wake wa karibu, KVZ kuendelea na matumaini ya kutwaa ubingwa huo, kwani endapo itashinda mchezo wake wa 22 dhidi ya Maafande wa Zimamoto, itakuwa pointi moja nyuma ya vinara hao wenye alama 47 huku KVZ ikiwa na mchezo mmoja mkononi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa KMKM, Ame Msimu, alisema kupoteza mchezo huo wa mbio za ubingwa haimaanishi wamekata tamaa ya kutetea taji hilo bali imewapa nguvu zaidi ya kupambana.

Alisema tangu awali alifahamu kuwa Ligi Kuu msimu huu imekuwa ya moto, hivyo kila mchezo wanaoshuka dimbani mapambano yanakuwa makali.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**ALLISTER AWANIWA CITY**
KLABU ya Manchester City inataka kumjumuisha kiungo wa kati wa Brighton na Argentina, Alexis Mac Allister mwenye umri wa miaka 24, kwenye kikosi chao msimu ujao. ***(Star)***

**LIVER WAKOMAA NA JUDE**
LIVERPOOL bado wanapambana kuwania kumsajili kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19. ***(CaughtOffside)***

**GIROUD LULU ENGLAND**
MSHAMBULIAJI wa AC Milan na Ufaransa, Olivier Giroud yuko tayari kurejea Ligi Kuu England huku klabu za London za West Ham, Fulham, Crystal Palace na Brentford zote zikimwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36. ***(Sun)***

**FRIMPONG AWINDWA UNITED**
KLABU ya Manchester United inapanga kumnunua beki wa kulia wa Bayer Leverkusen, Jeremie Frimpong, mwenye umri wa miaka 22. ***(Football Insider)***

**VEIGA ATAJWA ARSENAL**
ARSENAL imeungana na Manchester United katika kinyang'anyiro cha kuwania kumsajili kiungo wa kati wa Celta Vigo na Hispania, Gabri Veiga mwenye umri wa miaka 20. ***(AS, via Sun)***

**SANTOS KWA MKOPO**
CHELSEA itamruhusu kiungo wa kati wa Brazil, Andrey Santos mwenye umri wa miaka 18, kujiunga na Vasco da Gama kwa mkopo baada ya mkopo uliopendekezwa kwa Palmeiras kushindikana. ***(Fabrizio Romano)***

**SCOTT AFIKIRIWA NEWCASTLE**
KLABU ya Newcastle United inafikiria kumnunua kiungo wa Bristol City, Alex Scott mwenye umri wa miaka 19. ***(Sun)***

**KHEDIRA AFUATILIWA LIVER**
KLABU za Everton, Leicester City, Liverpool, Newcastle United, Tottenham Hotspur, West Ham United na Wolves zote zimekuwa zikimfuatilia kiungo wa kati wa Union Berlin, Mjerumani Rani Khedira, mwenye umri wa miaka 29. ***(90min)***

**WIRTZ ATAKIWA BARCA**
BARCELONA na Real Madrid zimefufua nia yao ya kutaka kumnunua kiungo wa kati wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Florian Wirtz, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 hivi majuzi akirejea uwanjani baada ya kuumia kwa muda mrefu. ***(Fijaches)***

**MAATSEN KUBAKISHWA**
KLABU ya Burnley inataka kumbakisha beki wa kulia wa Uholanzi, Ian Maatsen, mwenye umri wa miaka 20, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo kutoka Chelsea. ***(Sun)***

**BROZOVIV AGOMBEWA ULAYA**
KLABU za Chelsea, Barcelona na Real Madrid zinamfuatilia kwa karibu kiungo wa kati wa Inter Milan na Croatia, Marcelo Brozovic, 30. ***(La Gazzetta dello Sport)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA: MARTINELLI NI MASHINE ARSENAL

**Wakati mwingine lazima umpe mtu pumzi ili arudi na nguvu na shauku zaidi...**

**LONDON, England**

MIKEL Arteta anaamini kumpa dakika za kutosha Gabriel Martinelli kumempa Mbrazil huyo nguvu ya kufunga bao la ushindi kwa Arsenal katika mechi ya Leicester City, Jumamosi.

Katika mechi nne za awali za Arsenal, Martinelli alikuwa amebadilishwa na Leandro Trossard na katika ushindi wa 4-2 dhidi ya Aston Villa, aliingia akitokea benchi akichukua nafasi ya Mbelgiji huyo.

Wote walianza kwenye ushindi wa 1-0 katika Uwanja wa King Power ingawa alikuwa Martinelli aliyefunga bao pekee la ushindi katika dakika ya kwanza ya kipindi cha pili na kuimarisha nafasi ya Arsenal kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu.

"Wakati mwingine lazima umpe mtu pumzi ili arudi na nguvu na shauku zaidi," alisema Arteta kuhusu Martinelli ambaye amesaini mkataba mpya hadi mwaka 2027.

Arsenal walikuwa na wakati mgumu kwenye mchezo huo, lakini waliwazuia wenyeji na kupiga shuti moja tu kwa jumla na kutolenga lango.

Arteta alifurahishwa na ushindi huo, ambao uliongeza uongozi wa timu yake kileleni mwa ligi hadi pointi tano kabla ya ziara ya Manchester City dhidi ya Bournemouth juzi usiku.

Aliongeza: "Tulitawala mchezo tangu mwanzo hadi mwisho. Kwa ujumla, nadhani uchezaji wetu na uelewa wa nafasi ulikuwa bora.

"Tulikosa pasi hiyo ya mwisho ili kufunga zaidi. Kwa hakika wachezaji walijituma zaidi kwenye mchezo huu."

Vinara Arsenal wana mechi mbili za nyumbani wiki ijayo dhidi ya Everton na Bournemouth huku wakiwania taji la kwanza la ligi tangu mwaka 2004.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 490

MSHINDI WA SUPA JACKPOT YA MECHI - 13




PIGA *150*87#


Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RONALDO ATUPIA HAT-TRICK YA PILI AL NASSR




**RIYADH, Saudi Arabia**

CRISTIANO Ronaldo alikuwa na wakati mwingine mzuri kwenye Ligi Kuu ya Saudi Arabia, Saudi Pro League, kwa kufunga 'hat-trick' yake ya pili katika mechi tano alizocheza hadi sasa na kuipa Al Nassr ushindi wa 3-0 dhidi ya Damac, Jumamosi.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Real Madrid na Manchester United alikuwa ameshafunga mabao hayo matatu hadi mapumziko, huku akitoka kupachika manne wiki mbili zilizopita dhidi ya Al Wehda.

Bao la kwanza la Ronaldo dhidi ya Damac lilikuwa ni penalti ya dakika ya 18, iliyotolewa baada ya mpira wa mkono uliopigwa kwa Farouk Chafai, huku la pili likiwa ni shuti kali la mguu wa kushoto kutoka umbali wa yadi 20 dakika tano baadaye na bao la tatu alifunga dakika ya 44 akipokea pasi ya Ayman Yahya.

Yahya angeweza kupiga shuti na kufunga, lakini akachagua kumpasia Ronaldo mwenye umri wa miaka 38, na kupiga shuti akiwa umbali wa yadi 10.

Ronaldo amefunga hat-trick 44 katika maisha yake ya soka akiwa Madrid, na kuwa mfungaji bora wa wakati wote wa Klabu hiyo ya Hispania.

# Ancelotti: Mbio za ubingwa LaLiga ngumu

**MADRID, Hispania**

CARLO Ancelotti amekiri itakuwa "vigumu" kwa Real Madrid kushinda taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, baada ya 'Los Blancos' kulazimishwa sare ya bao 1-1 na wapinzani wao wa jiji moja, Atletico Madrid iliyokuwa na wachezaji 10.

Madrid wangefurahia nafasi yao ya kupunguza pointi hadi tano dhidi ya vinara Barcelona wakati mchezaji wa akiba wa Atleti, Angel Correa, alipotolewa kwa kadi nyekundu huku wakiwa hawajafungana, Jumamosi.

Atleti kisha walionekana kuwa tayari kupata ushindi wa kukumbukwa wakati Jose Gimenez alipowafunga kwa kichwa kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu, lakini mshambuliaji mwenye umri wa miaka 18, Alvaro Rodriguez ndiye aliyeokoa aibu ya Madrid kwa kusawazisha.

Huku mkwamo huo ukiipa Barcelona nafasi ya kusonga mbele kwa pointi 10 wakati jana Jumapili walipokuwa



wakicheza na Almeria Ancelotti anafahamu Madrid wana kazi ya ziada.

Alipoulizwa kuhusu mbio za ubingwa na DAZN, Ancelotti alisema: "Tayari ilikuwa ngumu sana kabla ya mechi hii, sasa ni zaidi. Tunaenda kupambana hadi mwisho, ndivyo ninavyoweza kusema.

"Tulikosa ari mpya. Lakini kiakili zaidi ya kimwili. Katika 1-0, ilituchukua dakika 10 kujipanga, kujiweka upya.

"Katika kipindi cha kwanza kulikuwa na ukosefu wa nguvu na cha pili, tulifikia mwisho, lakini hatukutumia kikamilifu ubora wa namba."

Hata hivyo, Ancelotti alimsifia Alvaro, ambaye alikuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kufunga katika mechi ya Madrid dabi kwenye LaLiga karne hii (umri wa miaka 18 na siku 226).

"Ilikuwa muhimu sana kwake, kijana mwenye ndoto kubwa ya kuichezea Real Madrid," alisema Ancelotti kuhusu fowadi huyo wa Uruguay.

"Huu utakuwa usiku maalum katika maisha yake."

Bao la kichwa la Alvaro dakika ya 85 lilimnyima Diego Simeone ushindi maarufu siku ambayo alifikia rekodi ya Luis Aragones ya mechi 612 akiwa kocha wa Atletico.

,825,190

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/02/22 | 22:45 | Preston vs Coventry | 2.46 | 3.19 | 2.70 |
| 02. 28/02/22 | 22:45 | Barrow vs Salford City | 2.46 | 3.15 | 2.90 |
| 03. 28/02/22 | 22:45 | Gillingham vs Bradford City | 2.85 | 3.15 | 2.46 |
| 04. 28/02/22 | 23:00 | Luton Town vs Millwall | 2.27 | 3.15 | 3.00 |
| 05. 01/03/22 | 19:00 | Slovacko vs Bohemians | 2.35 | 3.37 | 2.64 |
| 06. 01/03/22 | 19:00 | Farco FC vs Arab Contractors | 3.63 | 2.78 | 2.27 |
| 07. 01/03/22 | 20:00 | NK Osijek vs Hajduk Split | 2.69 | 3.11 | 2.46 |
| 08. 01/03/22 | 22:15 | FC Sion vs FC Lugano | 2.51 | 3.31 | 2.51 |
| 09. 01/03/22 | 22:15 | St. Gallen vs FC Basel | 2.26 | 3.48 | 2.70 |
| 10. 01/03/22 | 23:00 | Osasuna vs Athletic Bilbao | 2.98 | 2.98 | 2.48 |
| 11. 02/03/22 | 20:00 | Aalborg vs Viborg FF | 2.80 | 3.27 | 2.29 |
| 12. 02/03/22 | 22:45 | Royal Antwerp vs Union Saint Gilloise | 2.45 | 3.30 | 2.67 |
| 13. 02/03/22 | 23:00 | Real Madrid vs Barcelona | 2.51 | 3.34 | 2.65 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 27/02/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3689 | Bali Utd Pusam vs Persis Solo | 1.67 | 3.75 | 4.11 |
| 14:00 | 2984 | Bkma Yerevan vs Artsakh | 2.40 | 3.00 | 2.85 |
| 14:00 | 4697 | Oleksandria vs FC Metalist 1925 | 1.89 | 3.39 | 3.49 |
| 14:30 | 2003 | Zob Ahan vs Sanat Mes Kerman FC | 2.34 | 2.70 | 2.90 |
| 16:00 | 1456 | AL Hazm vs Hajer Club | 1.54 | 3.55 | 5.55 |
| 16:00 | 3206 | Singida BS FC vs Mtibwa Sugar | 1.74 | 3.08 | 4.72 |
| 16:00 | 4177 | Ghazl EL Mahallah vs Aswan | 2.67 | 2.87 | 2.77 |
| 16:05 | 5746 | Al Jabalain vs AL Qaisoma | 2.04 | 2.99 | 3.50 |
| 16:10 | 4799 | AL Ain vs Najran SC | 2.06 | 3.03 | 3.39 |
| 16:30 | 3622 | Apollon Limassol vs AEK Larnaca | 2.69 | 3.11 | 2.58 |
| 16:30 | 5527 | Persepolis FC vs Naft Masjed Soleyman FC | 1.62 | 3.36 | 5.37 |
| 17:00 | 1009 | Ararat Yerevan vs Ararat Armenia | 4.86 | 3.25 | 1.70 |
| 17:00 | 2283 | Ural Yekaterinburg vs Rostov | 2.33 | 3.12 | 2.86 |
| 18:00 | 2050 | Dinamo Bucuresti vs AFC Unirea Constanta | 1.08 | 9.02 | 14.35 |
| 18:30 | 2604 | Malkiya Club vs Al Ittifaq Bhr | 2.14 | 3.06 | 3.26 |
| 18:30 | 3071 | Qalali vs AL Ittihad Bhr | 2.80 | 2.95 | 2.48 |
| 18:30 | 5953 | Bouri vs Busaiteen | 3.53 | 3.32 | 1.94 |
| 19:00 | 2421 | Karabakh vs Neftchi Baku | 1.48 | 3.94 | 5.81 |
| 20:00 | 3153 | Tunisia vs Zambia U20 | 1.97 | 3.11 | 3.68 |
| 20:00 | 3236 | Talaea El Gaish vs El Ittihad Alexandria | 2.74 | 2.79 | 2.84 |
| 20:00 | 3636 | Spartak Moscow vs Lokomotiv Moscow | 1.76 | 3.42 | 4.15 |
| 20:00 | 3908 | SC Kfar Qasem vs Ahi Nazareth | 2.56 | 2.96 | 2.85 |
| 20:00 | 4362 | Maccabi Jaffa vs Nazareth Ilit | 2.11 | 3.27 | 3.32 |
| 20:00 | 4851 | Gambia vs Benin | 2.49 | 2.79 | 2.94 |
| 20:00 | 4895 | El Fahem vs Ironi Hasharon | 2.03 | 3.06 | 3.85 |
| 20:00 | 5162 | Nieciecza KS vs Skra Czestochowa | 1.49 | 3.90 | 5.54 |
| 20:30 | 1071 | Degerfors vs Skovde Aik | 1.52 | 3.99 | 5.18 |
| 20:30 | 3242 | IFK Luleaa vs Malmo | 27.06 | 8.95 | 1.05 |
| 20:30 | 4084 | Verona vs Fiorentina | 3.09 | 3.19 | 2.21 |
| 21:00 | 1726 | Zaglebie Lubin vs Miedz Legnica | 2.05 | 3.13 | 3.29 |
| 21:00 | 3550 | Petrolul Ploiesti vs CFR Cluj | 5.02 | 3.40 | 1.67 |
| 21:00 | 4261 | Midtjylland vs Brondby | 2.03 | 3.48 | 3.38 |
| 21:00 | 4550 | Hapoel Beer Sheva vs Maccabi Bney Reine | 1.24 | 4.82 | 10.26 |
| 21:00 | 4827 | Viktoria Koln vs Freiburg II | 2.38 | 3.23 | 2.86 |
| 21:00 | 5218 | Szeged vs Bgsz Siofok | 1.75 | 3.34 | 4.21 |
| 21:30 | 3221 | Audax Rio EC RJ vs Madureira RJ | 2.30 | 2.95 | 3.06 |
| 22:00 | 3078 | Sporting Lisbon vs GD Estoril | 1.21 | 6.13 | 10.87 |
| 22:00 | 4568 | Maastricht vs PEC Zwolle | 4.89 | 4.68 | 1.48 |
| 22:00 | 5465 | Jong PSV vs Jong AZ Alkmaar | 2.26 | 3.38 | 2.81 |
| 22:30 | 4747 | Feralpisalo vs Pordenone | 2.72 | 2.99 | 2.72 |
| 22:45 | 2120 | Lazio vs Sampdoria | 1.40 | 4.24 | 7.11 |
| 22:45 | 3588 | Amiens vs Bordeaux | 2.79 | 3.23 | 2.43 |
| 23:00 | 1743 | FC Aguablanca vs Leones FC | 2.53 | 3.00 | 2.69 |
| 23:00 | 1816 | Villarreal vs Getafe | 1.63 | 3.56 | 5.35 |
| 23:00 | 2602 | Barracas Central vs Gimnasia y Esgrima | 2.52 | 2.95 | 2.75 |
| 23:00 | 3486 | FC Versailles 78 vs Concarneau | 2.68 | 3.26 | 2.46 |
| 23:00 | 4426 | Swansea vs Rotherham | 1.54 | 3.87 | 5.49 |
| 23:00 | 5110 | Puerto Nuevo vs CA Atlas | 2.59 | 2.80 | 2.80 |
| 23:00 | 5530 | Granada vs Malaga | 1.56 | 3.64 | 5.70 |
| 23:30 | 5353 | Academia Cantolao vs Cusco FC | 2.66 | 3.23 | 2.36 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# TANGA CEMENT NA MIAKA 20 UDHAMINI KILI MARATHON

**Na Mwandishi Wetu**

SIMBA Cement imeendelea kuwa kinara wa ufadhili wa mbio za Kili Marathon kwa miaka 20 sasa huku ikielezwa kuwa mbio hizo za kimataifa zimezidi kuboreshwa zaidi kila mwaka.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mbio hizo zilizofanyika za mwaka huu zilizofanyika jana Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, Meneja Biashara wa Tanga Cement PLC, Peet Brits, alisema, huu ni mwaka wa 20 wa ushiriki wao wakiwa wadhamini wakongwe na wakimbiaji kupitia timu za Simba katika mbio hizo ambazo Simba Cement na waandaaji wa Kili Marathon wamekuwa wakiziboresha hadi kufikia miaka 21 kwa mwaka 2023.

Alisema, udhamini wa mbio hizo ni kutokana na umuhimu wa michezo hasa Kili Marathon ambayo huwakutanisha wafanyakazi wa Simba Cement na kufanya shughuli hii kwa umoja kama wanavyofanya viwandani pamoja kukutana na wadau pamoja na wateja wao.

"Katika ushiriki wetu hatukuangalia vyeo au nafasi zetu za kazi, tuliona mkurugenzi mtendaji akigawa maji kwa wakimbiaji...tulizungumza lugha moja kutoka langoni hadi kileleni kwa ushirikiano na wafanyakazi ambao ni wakimbiaji (Timu Simba,) kwa pamoja na wakimbiaji wengine, wadau na wateja," alisema.

Pia, alisema, baada ya mbio hizo wafanyakazi ambao ni wakimbiaji wamekutana na wateja na wadau wao Kanda ya Kaskazini na kubadilishana mawazo ya uboreshaji katika huduma.

Kuhusiana na mafanikio kupitia mbio za Kili Marathoni, Peet alisema, wamefurahi kushirikiana katika mbio hizo zilizofanyika kwa mara ya 21 sasa na kufanya vizuri katika mbio hizo pamoja na kutoa huduma ya kugawa maji kwa wakimbiaji wa Kilometa 42 na 21 waliopita katika kituo chao cha kugawia maji.

"Tuna uhakika wakimbiaji wamefurahi kupita katika kituo chetu cha Point 8 wakati wa mbio hizi na kupata huduma, tutaendelea kushiriki katika tukio hili kila mwaka...tunaipenda na kuithamini Kili Marathon na tunafurahi kudhamini kwa kugawa maji kwa wateja wetu na wadau wote waliopita katika 'Water Point' yetu na hawa ni kutoka katika Kaskazini ambayo ni Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga na mikoa mingine," alisema.

Aidha, alisema kwa mwaka huu walijipanga kufanya vema zaidi ikilinganishwa na uliopita kwa kuongeza idadi ya wakimbiaji kwa timu ya Simba Cement pamoja na kuongeza nguvu baina yao kwa kuwapa moyo wakimbiaji na kumaliza kwa ushindi.

Peet alisema, kwa mwaka huu wamevunja rekodi kwa kuwa na jumla ya washiriki 28 na kupitia Kili Marathon wamesherehekea kwa upekee mafanikio ya mwaka 2022 wakiwa washindi wa jumla wa tuzo ya Rais kwa mzalishaji bora wa mwaka na mshindi wa jumla wa tuzo ya taarifa ya fedha iliyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA).



Meneja Masoko na Mawasiliano wa Tanga Cement PLC, Mtanga Noor, akihudumia vinywaji kwa baadhi ya wakimbiaji wa kilomita 42 na 21 waliokuwa wakipita kwenye kituo cha maji na soda cha Simba Cement wakati wa mbio za Kili Marathon zilizofanyika mwishoni mwa wiki mjini Moshi mkoani Kilimanjaro. **MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake Watanzania

INATOKA UK. 24

Naibu Waziri alisisitiza kwamba serikali itaendelea kutoa ushirikiano pale unapohitajika kuhakikisha mbio hizo zinazidi kuwa kubwa na kushirikisha watu wengi zaidi kutoka ndani na nje.

Wakizungumza baada ya mbio hizo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bia ya Kilimanjaro, Jose Moran, alishukuru viongozi na wakazi wa Moshi kwa ushirikiano mkubwa ulitolewa kufanikisha mbio hizo ambazo sasa zimetimiza miaka 21.

Wadhamini wa mbio za mwaka huu ilikuwa ni pamoja na Kilimanjaro Premium Lager-42km (Wadhamini Wakuu), Tigo- 21km Nusu Marathon, Grand Malt – 5Km Mbio za Furaha, wadhamini wa meza za maji walikuwa ni TPC Sugar, Simba Cement, Kilimanjaro Water, Total-Energies na watoa huduma rasmi Surveyed Plots Company Limited (SPC) Kibo Palace Hotel, CMC Automobiles, KK Security na Keys Hotel.

Kili Marathon huandaliwa na Kilimanjaro Marathon Company Limited na kitaifa inaratibiwa na Executive Solutions Limited.

# ROBERTINHO AANIKA

INATOKA UK. 24

tulizijua mbinu zao tukafanikiwa kuwadhibiti," alisema Robertinho.

Beki wa Simba, Joash Onyango alisema kikubwa walipambania ni kutafuta matokeo katika mchezo huo na kufanikiwa kuvuna pointi tatu ugenini.

"Tulihitaji pointi tatu kabla ya hii mechi, kama wachezaji tulikaa na kuzungumza kwa kila mmoja kujipa majukumu ya kuhitaji kupambana na kulazimika kurejea na pointi muhimu na hili tumefanikiwa na tumerejea nyumbani kwa maandalizi ya mechi zetu zijazo," alisema Onyango.

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema baada ya kufika Dar es Salaam jana wachezaji wamepewa mapumziko ya siku moja kwenda nyumbani kukutana na famili zao na kupumzisha miili na akili kutokana na kazi ngumu waliyofanya.

"Timu itarejea mazoezi kesho (leo) Jumatatu kujiandaa na mchezo wa hatua ya 16-bora wa Kombe la Shirikisho la Azam dhidi ya African Sports kutoka Tanga," alisema Ahmed.

# Michezo

Jumatatu Februari 27, 2023

Nipashe





UKURASA 21

## Arteta: Martinelli ni mashine

POOZA KOO...




Wanariadha wakipata huduma ya maji katika meza ya Kampuni ya Maji ya Kilimanjaro kwenye mbio za Kili Marathon zilizofanyika mjini Moshi jana. Kilimanjaro Water, ni miongoni mwa wadhamini wa mbio hizo ambazo hufanyika kila mwaka mkoani Kilimanjaro. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# ROBERTINHO AANIKA SIRI KUICHAPA VIPERS

## ●●●Asema moto sasa umewaka Simba akiisubiri tena kwa Mkapa huku akitaja...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuvuna pointi tatu ugenini dhidi ya Vipers, Kocha Mkuu wa Simba, Robertiho Oliveira, ametambia mfumo mpya kuwasaidia kuibuka na ushindi huku akieleza matokeo hayo yamerudisha uhai mpya katika mipango yao ya kusaka pointi sita za michezo miwili ya nyumbani.

Amesema amefurahishwa na kiwango kizuri cha wachezaji wao walichokionyesha katika mchezo wa tatu wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Vipers na kufanikiwa kuibuka na ushindi wa bao 1-0 Uwanja wa St Mary's, Uganda bao pekee likifungwa na beki Henock Inonga baada ya mpira wa faulo uliopigwa na Mohamed Hussein 'Tshabalala' na kuchezwa kwa kichwa na Sadio Kanoute kisha Moses Phiri kabla ya mfungaji kuuzamisha nyavuni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Robertinho alisema kilichomfurahisha ni jinsi walivyocheza kitimu hasa kipindi cha pili huku muunganiko wa wachezaji vijana na wazoefu ukiwa mzuri.

"Wiki hii (iliyopita) yote nilikuwa na kazi ya kubadilisha mfumo wa uchezaji na umeniletea matokeo chanya, nilijua timu yangu ya zamani ina wachezaji wazuri sana, wanacheza mfumo wa 4-3-3 na mimi nimetumia 4-4-2, lakini nimetumia wachezaji vijana kushambulia kama Kibu, Moses Phiri, tumefunga bao moja na kupoteza nafasi mbili ndani ya eneo la hatari, na nimejaribu kuchanganya wachezaji wazoefu na damu changa," alisema kocha huyo.

Alisema jambo jema kwao ni kupata matokeo mazuri katika mchezo muhimu na kurejea nyumbani na pointi tatu bila kujali wameshinda bao ngapi.

"Katika Ligi ya Mabingwa hasa hatua ya makundi ushindi ndio jambo linalotakiwa, iwe moja, mbili au nne kinachoangaliwa ni pointi tatu.

"Tumecheza vizuri, tulikuwa na muunganiko mzuri mbinu yetu ilikuwa kuhakikisha tunapata ushindi kipindi cha pili muunganiko wetu uliimarika, kasi iliongezeka iliyochangiwa na wachezaji vijana na wazoefu," alisema Robertinho.

Alisema kuhusu viwango vya wachezaji wao wamepambana kwa kucheza kufa kupona katika mchezo ngumu na ushindani mkubwa ambao matokea hayo yameifanya timu hiyo kufufuka kuelekea katika michezo yao miwili watakaocheza nyumbani kuvuna pointi sita.

Kuhusu kiwango cha Denis Kibu alisema ni mchezaji mzuri na katika mchezo huo ameitendea haki nafasi aliyompa kwa kufuata aliyomwelekeza katika mazoezi kwa kuhamishia kwenye mechi.

Kocha huyo alisema benchi la ufundi lina kazi kubwa kuwajenga kisaikolojia wachezaji wake akiwamo Kibu kuonyesha kile alichonacho ili kuwa bora zaidi.

"Haikuwa mechi rahisi, Vipers walikuwa washindani wamecheza vizuri, lakini

INAENDELEA UK. 23

## Wanawake Watanzania watamba Kili Marathon

**Na Mwandishi Wetu**

SARAH Ramadhan ameibuka mshindi wa Mbio za Kimataifa za Kilimanjaro Lager Marathon za kilomita 42 akifuatiwa kwa mbali na Watanzania wenzake wawili kukamilisha ushindi wa kishindo kwa mara ya kwanza wa wanawake kwenye mashindano hayo.

Sarah, ambaye alimalizia mbio hizo akiwa na tabasamu kubwa usoni huku akishangiliwa kwa nguvu na uwanja mzima, alitumia muda wa saa 3:02:36 kutwaa ushindi huo wakati mbio hizo zikiadhimisha miaka 21 tangu kuanzishwa kwake zilizofanyika jana kwenye Uwanja wa Chuo Kikuu cha Ushirika mjini Moshi.

Nafasi ya pili ilichukuliwa na Neema Sanka aliyetumia muda wa saa 3:20:05 akifuatiwa na Visa Androd Mhalwa katika nafasi ya tatu ambaye alitumia muda wa saa 3:25:14.

Mbio hizo kwa miaka mingi zimekuwa zikitawaliwa na wanariadha kutoka Kenya, lakini jana walijikuta wakikosa nafasi zote tatu za juu huku Mathange Jane akiwa katika nafasi ya nne.

Hata hivyo, kwa upande wa wanaume, Wakenya waliendelea kuwa tishio kwani Kenneth Kiprop Omulo, aliibuka mshindi akiwa ametumia muda wa saa 2:18:05 akifuatiwa kwa karibu na Mtanzania Aloyce Simbu aliyetumia muda wa saa 2:18:29. Nafasi ya tatu katika mbio hizo ndefu za kila mwaka ilichukuliwa na Mkenya mwingine Abraham Kipkosgei Too aliyetumia muda wa saa 2:19:30.

Kwa ushindi huo, Sarah alijipatia shilingi milioni 4.2 taslimu kama zawadi iliyoahidiwa kwa kila atakayeibuka mshindi wa kwanza kwa pande zote mbili za mbio za wanaume na wanawake na wadhamini wakuu Kilimanjaro Lager na pia zawadi ya ziada ya milioni 1.5 kwa kuwa Mtanzania aliyeongoza kwenye mbio hizo.

Simbu aliyeshika nafasi ya pili kwenye mbio hizo za kilomita 42 kwa wanaume, alijichukulia shilingi milioni 2.1 na pia zawadi ya ziada ya shilingi milioni 1.5 kwa kuwa Mtanzania aliyeongoza kwenye mbio hizo.

Akizungumza wakati wa shughuli za utoaji zawadi, Naibu Waziri wa Utalii, Mary Masanja, ambaye alimwakilisha Waziri wa Utalii Mohamed Mchengerwa, alishukuru ushirikiano uliofanya kufanikiwa kwa mbio hizo ambazo kwa kiasi kikubwa zinautangaza Mlima Kilimanjaro na sekta ya utalli kwa ujumla nchini.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >